epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatatu Julai 15, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581738
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 21

**RUDIGER APEWA OFA YA BEKI GHALI ZAIDI DUNIANI**

## WATOTO WAJIFUNGUA
# Samia akuna kichwa, aonya

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akiangalia watoto njiti waliowekwa katika chumba maalum ili wakue na kuimarika alipotembelea Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Katavi jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA WA 2

**Mbowe:** Miradi inatekelezwa kwa fedha za wananchi, si hisani bali wajibu

UKURASA WA 3

**CCM** yaagiza wafanyabiashara wote Kariakoo iliyoungua sasa warejeshwe

UKURASA WA 3

**Wananchi** walia kucheleweshewa huduma ya maji, vigogo DAWASA wapewa angalizo

## Trump apigwa risasi, ashukuru FBI kwa kumnusuru

UKURASA 19

# CWT yabaini shida nyingine kwenye kikokotoo cha mafao

UKURASA 5

**MICHEZO** GAMONDI AWATUMIA UJUMBE KINA CHAMA UK.24

**KATUNI** UK.6



Baadhi ya wanachama wa vilabu vya Rotary Tanzania wakiwa wamebeba miche ya miti kwa ajili ya uzinduzi wa kampeni ya kupanda miti zaidi ya 30,000 kwa mwaka, uliofanyika katika Shule za Msingi Mtakuja na Mtongani Kinondoni jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, ikiwa ni maadhimisho ya miaka 100 ya shughuli za Rotary katika nchi za ukanda wa Afrika Mashariki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia akuna kichwa watoto kujifungua

**Na Neema Hussein,** KATAVI

WATOTO wamejifungua watoto: Sasa wanabeba majukumu yanayokiuka sheria - mtoto kulea mtoto mwenziwe; Sheria ya Ulinzi wa Mtoto, 2009 imekiukwa.

Ni jambo lililomshtua Rais Samia Suluhu Hassan jana alipobaini kuwapo idadi kubwa ya watoto wanaojifungua wakiwa chini ya umri wa miaka 19 mkoani Katavi.

Baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Katavi na kutembelea wodi ya wazazi ya hospitali hiyo, Mkuu wa Nchi alibaini kuwapo wazazi waliojifungua ambao wana umri wa kati ya miaka 15 na 19.

"Wakati ninatembea kwenye hospitali hii, nilipita kwenye wodi ya kinamama wanaojifungua na hasa wale watoto ambao hawajatimia (njiti).

"Nimekuta mama mmoja tu ndiye aliyepevuka, ana miaka 22, lakini wengine wote wapo kati ya miaka 15 na 19 na hawa ndio wanajifungua watoto ambao hawajatimia.

"Ninaomba sana wananchi wa mkoa huu wa Katavi, wapeni nafasi watoto wa kike waweze kusoma na kutimiza malengo yao na hata wafikie umri unaostahili angalau ajifungue akiwa amefikia umri wa miaka 19 na kuendelea, siyo hali hii niliyoikuta hapa, hii siyo sawa.

"Ujumbe huo ni kwenu wananchi mliopo hapa na wale ambao wananisikiliza kupitia vyombo vya habari, tujitahidi kuwapa nafasi watoto wa kike wapate elimu, wapevuke kabla ya kuolewa au kupewa ujauzito, hilo ninaomba sana sana," Rais aliagiza.

Sheria ya Ulinzi wa Mtoto, 2009 inazuia mtoto (umri chini ya miaka 18) kutekeleza majukumu ya mtu mzima.

Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inazuia mtoto chini ya miaka 15 kuolewa, hivyo alichobaini Rais Samia jana kinakinzana na sheria.

Rais Samia pia alipongeza alichokitaja "kazi nzuri iliyofanywa kwa kujenga hospitali inayokidhi vigezo vya kuwa ya rufani".

Kwa mujibu wa Rais Samia, hospitali hiyo ina vifaa vya kisasa sawa na hospitali za rufani zilizoko Mwanza, Dar es Salaam na maeneo mengine nchini, hivyo huduma zinazotolewa katika hospitali hiyo zitapunguza gharama za kusafiri kutafuta huduma za afya.

"Pamoja na mambo ambayo nimeyasema, niwapongeze kwa kazi kubwa iliyofanyika katika hospitali hii. Nimeona vifaa vya kisasa kabisa vipo hapa ambavyo tulikuwa tumezoea kuviona katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha.

"Kwa sasa vifaa hivyo vipo hapa Katavi, hii itasaidia kupunguza gharama za wananchi kusafiri umbali mrefu kutafuta huduma ya afya," alisema.

Rais Samia pia aliwataka wananchi kujiunga na bima ya afya ili kuwapunguzia gharama za matibabu.

Rais Samia pia alizindua jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Mkoa wa Katavi lililogharimu zaidi ya Sh. bilioni 1.4. Alisema serikali itaendelea kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Kuboresha Mifumo ya Haki Jinai, ikiwamo kuboresha miundombinu ya Jeshi la Polisi na vituo vyake pamoja na utendaji wa watumishi.

Alipongeza jeshi hilo kwa kuendelea kutunza usalama katika Mkoa wa Katavi licha ya kuwa na mwingiliano wa watu kutoka nje ya mkoa huo sambamba na kuimarisha usalama wa kisiasa ndani ya mkoa.

Vilevile, Rais Samia alizindua ujenzi wa maghala na vihenge vya kisasa vya kuhifadhi nafaka, akielekeza Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kuwezesha Mkoa wa Katavi kuwa kanda inayojitegemea kwenye ununuzi na uhifadhi wa nafaka.

Sambamba na hiyo, Rais Dk. Samia alizindua msimu mpya wa ununuzi wa nafaka kwa mpaka 2024/25 katika maghala ya NFRA yaliyoko Manispaa ya Mpanda, mkoani Katavi na kutaka wanunuzi kuzingatia haki wakati wa ununuzi na kuwapatia wakulima bei nzuri ya mazao.

Mradi huo utasaidia nchi kuwa na uhakika wa chakula na kupunguza upotevu wa chakula baada ya kuvunwa na utaongeza uhifadhi wa nafaka kwa Mkoa wa Katavi kutoka tani 5,000 hadi 28,000.


## TANGAZO LA MNADA

Freemind, **Arm na Rapitech** Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya Mnada Jijini Dar es salaam Mteja anashauriwa kulipa deni ndani ya siku 14 za hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe ya Mnada inavyoonekana hapa chini.

| | Jina la Mteja | Aina ya Gari | Dalali | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Rhoda Asante Shilesaryo | Toyota hilux T553ALR | Freemind | 30.07.2024 |
| 2 | Damas Mukassa Kasheegu | BMW T431 DDR | ARM Auctioneer | 30.07.2024 |
| 3 | Hussein Mhini Hussein | Toyota Gaia T843BSV | Freemind | 30.07.2024 |
| 4 | Graceana January Mndewa | Toyota Ractis T321DKR | Rapitech | 30.07.2024 |

**Masharti ya Mnada.**

1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25% (au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%) litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe yaTangazo.

**Kwa Mawasiliano Piga 0677014355(Fanikiwa)**


# Mbowe: Miradi inatekelezwa kwa fedha za wananchi

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesema fedha za utekelezaji miradi ya maendeleo ni za walipakodi na serikali inapotekeleza ni wajibu wake na si hisani.

Akizungumza jana katika Kata ya Nasai, Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, Mbowe alisema fedha za kujenga madarasa, zahanati, shule na barabara ni za wananchi, serikali ikijenga si fadhila kwao, bali ni wajibu wake.

Mbowe na Godbless Lema, Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini, wako katika mwendelezo wa operesheni maalum iliyobatizwa jina la 'Operesheni GF' katika majimbo 35 ya mikoa ya kaskazini mwa nchi.

"Maendeleo ya watu na ninasisitiza; maendeleo ya watu ni uchumi wa watu. Ili uchumi wa watu uweze kuongezeka ni lazima uchumi wa nchi upanuke. Uchumi wa nchi unapauliwa na uchumi wa mtu mmoja mmoja.

"Rais wa nchi hana senti tano yake. Fedha zozote ambazo Rais, serikali inaamua kuzitumia, wanaopitisha mapato na matumizi ya serikali ni Bunge.

"Na ndani ya Bunge wanajadili mapato na matumizi. Rais anapelekewa bajeti, kitu kinachoitwa Finance Bill (Muswada wa Sheria ya Fedha) anautia saini kuwa sheria. Baada ya Bunge kupitisha na Bunge ndugu zangu wa Siha, Bunge halina fedha zake," alisema.

Mbowe alisema fedha ambazo Bunge linaidhinisha matumizi na mapato ni fedha za kodi, akimnukuu Waziri Mkuu wa zamani wa Uingereza, Magreth Thatchar, "There is nothing like government money, is always tax payer money (hakuna fedha za serikali, siku zote ni fedha za mlipakodi)".

"Hizi fedha za kujenga madarasa, kujenga zahanati, kujenga shule, kujenga barabara; serikali ikijenga si fadhila kwenu, ndiyo haki yake, ni wajibu wake ambao wamechelewa kuutekeleza.

"Leo tuna miaka 63, kwanini tuna shida ya madarasa? Sijui mnanielewa ninyi wa Siha nyie! Hebu fikiria wilaya nzima ya Siha hii haina kiwanda hata kimoja, lakini kila mwaka tunazalisha vijana wanaomaliza shule.

Hawa vijana tunawapeleka wapi na serikali ina mpango gani?

**LEMA NA CHAWA**

Awali katika mkutano huo Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini, Lema, alisema hakuna kizazi kimekuja kuwa hakina majukumu ya msingi kama hiki cha sasa.

"Kizazi chetu, kizazi hiki kingekuwapo wakati Nyerere anapigania uhuru, Tanzania bado ingekuwa kwa mkoloni. Kimekuwa ni kizazi cha 'machawa', wapambe, walaghai na waoga," alilalama Lema.

Alisisitiza kuwa, "kuna gharama usipolipa mzazi atalipa mtoto wako, sasa ninyi mnaweza mkawa hamjipendi, lakini fikiria maisha ulinayonayo wewe, halafu fikiria mtoto wako ataishije. Vijana wote nchi nzima leo, ajira yao ni bodaboda na kukata loku (kunywa pombe kali).

"Asilimia 80 au 90 ya vijana wanaomaliza shule za msingi, sekondari mpaka chuo kikuu wako mitaani. Vijana wengi waliokuwa wagonjwa wa figo na ini ni kwa kunywa pombe kupindukia kwa sababu ya ugumu wa maisha."

HABARI KITAIFA

# DAWASA yaikera CCM, Makalla awapa angalizo

Na Romana Mallya

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imemkera Katibu wa NEC -Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Amos Makalla:

Wananchi waliolipa fedha kuunganishiwa maji na mamlaka hiyo, hawajapatiwa huduma hiyo kwa muda mrefu.

Makalla amesema alipata malalamiko kuhusu ugawaji vifaa kwa wananchi waliolipia maji, lakini baada ya kusikia atafanya ziara huko wamewahi kwa kuanza kuvigawa.

Amesisitiza kuwa hatopenda kuona tena yaliyotokea wiki iliyopita mpaka wasukumwe na Waziri wa Maji, Jumaa Aweso na mabadiliko aliyofanya ndipo wafanye kazi.

Makalla aliyasema hayo jana wakati akikagua mradi wa tangi la maji la Mshikamano, wilayani Ubungo, ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake mkoani Dar es Salaam.

Katika ziara hiyo, Makalla pia alitembelea shule ya sekondari ya mchepuo wa sayansi (Dar es Salaam Girls High School) iliyoko wilayani Ubungo ambayo ni miongoni mwa zinazojengwa kwa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan na kuwataka wanafunzi kutimiza ndoto ya Mkuu wa Nchi kwa kutopata mimba au kuwa watoro.

Akiwa kwenye mradi wa maji, Makalla alisema wakati huo walipompa taarifa Rais Samia kuhusu historia ya maji mkoani humo, upatikanaji wake ulikuwa wa asilimia 90 na kuagizwa itafsiriwe ili walioko pembezoni mwa mji wajue nao ni sehemu ya mkoa huo.

Alisema Rais Samia alipotoa fedha za UVIKO-19 zilipelekwa pia katika mradi huo ili wananchi wapate huduma ya maji.

"Maelekezo ya CCM ni kuhakikisha wananchi wanapata maji. Kazi tunayowaachia mmeniambia eneo lililobaki kupata maji Jimbo la Kibamba ni Msumi.

"Mmeeleza mnachimba visima vitatu na mna mpango wa muda mrefu wa kujenga tangi, ufanyike haraka wananchi wapate maji.

"Watendaji mkianza kulegea hamjui pampu kama zinafanya kazi, hamjui kama maji yanaingia katika tangi wala kama wananchi wanapata maji, hilo ni tatizo," alisema.

Makalla aliagiza wananchi wanapolipa ili kuunganishiwa maji wasichelewesheshewe, wapatiwe huduma haraka.

Awali Mbunge wa Kibamba, Issa Mtemvu, alisema eneo ambalo halijapata maji jimboni humo ni Kata ya Mbezi, Mtaa wa Msumi.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Ubungo, Rogati Mbowe, alisema Waziri Aweso amefanya "maajabu makubwa Ubungo" na wananchi wamefurahi kwa kuwa walikuwa wanapigwa danadana.

# ...CCM yaagiza wafanyabiashara wote Kariakoo iliyoungua warejee

Na Romana Mallya

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimeagiza ugawaji vibanda Soko Kuu la Kariakoo ufanyike kwa uwazi kwa kila aliyekuwamo katika daftari la orodha na anakidhi vigezo vyote.

Katibu wa NEC - Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM, Amos Makalla, alieleza hayo jana wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika Kituo Kikuu cha Mabasi Magufuli wilayani Ubungo, ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake mkoani humo kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo.

"Tuliahidi na CCM ikiahidi inatekeleza. Kama Katibu Mwenezi kwa niaba ya CCM niwaelekeze mamlaka, Meneja wa Soko la Kariakoo, hivi yupo hapa? Tulimwambia aje hapa, hajaja.

"Mkuu wa Wilaya yupo, maelekezo umeyasikia, hatutaki kusikiliza tena minong'ono na maandamano ya waliokuwa wafanyabiashara wa Soko la Kariakoo.

"Wapewe kipaumbele wale wanaostahili kwa idadi ile ambayo tutaihakiki ili kuondoa manung'uniko, ni watu wema wametuvumilia, wamekuwa pembeni siku zote, soko limekamilika wapewe kipaumbele kufanya biashara," aliagiza.

Makalla alikumbusha kuwa alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, hivyo anajua historia ya soko hilo lilipoungua. "Soko lilipoungua hakuna siku nilipata shida kama wakati ule. Nilipewa taarifa soko linaungua, dereva anakaa Chanika, mimi nipo Masaki, nilijiendesha mwenyewe.

"Nilishiriki kuzima moto haikuwezekana. Waziri Mkuu (Kassim Majaliwa) alikuja siku ya pili. Wananchi wameshachanganyikiwa, walihitaji maneno mazuri ya faraja.

"Mimi kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan niliwaambia kwa muda huo nitawapeleka Soko la Kisutu na Soko la Machinga Complex na Rais akatoa fedha kuboresha Soko la Machinga Complex," alisema.

Makalla alisema ahadi aliyotoa kama Mkuu wa Mkoa wakati ule ni kipaumbele kwa waathirika waliokuwapo wakati soko linaungua.

"Huo ndio ulikuwa mwanzo wa wananchi kutuelewa na Rais Samia akatoa Sh. bilioni 28, hivyo soko linakwenda kukamilika.

"Hatua ambayo Mkuu wa Mkoa aliyochukua ya kufuta majina 891 ni sahihi ili wananchi walioondoka 1,662 hatutaki waonewe, kila aliyeondoka wakati soko linaungua apate haki yake ya kurudi, wahakikiwe! Hatutaki manung'uniko," aliagiza.


Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

# PRESIDENT'S OFFICE-REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

# USHETU DISTRICT COUNCIL

## THE FINANCIAL STATEMENTS FOR THE USHETU DISTRICT COUNCIL FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2023

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT OFFICE -REGIONAL ADMINISTRATIVE AND LOCAL GOVERNMENT
00833118 - USHETU DISTRICT COUNCIL

### STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 30 JUNE 2023

| | Note | 2023 (TZS) | Restated 2022(TZS) |
|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | |
| **Current Asset** | | | |
| Cash and Cash Equivalents | 62 | 1,906,678,113 | 579,337,943 |
| Receivables | 67 | 324,333,297 | 932,837,810 |
| Prepayments | 69 | 672,659,141 | 860,319 |
| Inventories | 70 | 588,171,189 | 664,686,739 |
| Other Financial Assets | 71 | 36,000,000 | 36,000,000 |
| **Total Current Asset** | | **3,527,841,740** | **2,213,722,812** |
| **Non-Current Asset** | | | |
| Property, Plant and Equipment | 77 | 21,627,968,200 | 15,517,342,488 |
| Work In Progress | 82 | 6,214,696,534 | 6,711,257,346 |
| Total Non-Current Asset | | 27,842,664,734 | 22,228,599,834 |
| **TOTAL ASSETS** | | **31,370,506,474** | **24,442,322,647** |
| **LIABILITIES** | | | |
| Current Liabilities | | | |
| Payables and Accruals | 89 | 2,173,689,998 | 1,894,911,319 |
| Deferred Income | 93 | 1,414,411,355 | 693,140,634 |
| Deposits | 94 | 244,320,135 | 10,539,703 |
| Total Current Liabilities | | 3,832,421,488 | 2,598,591,655 |
| Non-Current Liabilities | | | |
| Other Borrowings by Government Entities | 102 | 172,157,700 | 259,850,000 |
| **Total Non-Current Liabilities** | | **172,157,700** | **259,850,000** |
| **TOTAL LIABILITIES** | | **4,004,579,188** | **2,858,441,655** |
| **Net Assets** | | **27,365,927,286** | **21,583,880,991** |
| NET ASSETS | | | |
| Other Reserves | | 36,000,000 | 36,000,000 |
| Accumulated Surpluses/Deficits | | 27,329,927,286 | 21,547,880,991 |
| **TOTAL NET ASSETS** | | **27,365,927,286** | **21,583,880,991** |

**Hadija M. Kabojela**
**District Executive Director**
Date: 23/3/2024

**Hon. Gagi L. Gagi**
**Council Chairman**
Date: 23/3/2024

23 MAR 2024 — USHETU DISTRICT COUNCIL

Controller and Auditor General — AR/LGA/83/3118/2022/23

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT OFFICE -REGIONAL ADMINISTRATIVE AND LOCAL GOVERNMENT
00833118 - USHETU DISTRICT COUNCIL

### STATEMENT OF FINANCIAL PERFORMANCE FOR THE PERIOD ENDED 30 JUNE 2023

| | Note | 2023 (TZS) | Restated 2022 (TZS) |
|---|---|---|---|
| **Classification of Expenses by Nature** | | | |
| **Revenue** | | | |
| Revenue from Exchange Transactions | 17 | 831,835,965 | 1,306,808,670.10 |
| Levies | 18 | 288,603,169 | 1,179,632,227.46 |
| Fees, Fines, Penalties and Forfeits | 19 | 283,343,809 | 142,090,138.00 |
| Social Contributions (Revenue) | 20 | 206,384,668 | 266,192,787.68 |
| Other Revenue | 31 | 146,326,100 | 7,498,100.00 |
| Subvention from other Government entities | 32 | 31,750,407,225 | 29,622,984,909.91 |
| **Total Revenue** | | **33,506,900,936** | **32,525,206,833.15** |
| **EXPENSES AND TRANSFERS** | | | |
| **Expenses** | | | |
| Wages, Salaries and Employee Benefits | 34 | 20,467,535,556.46 | 18,204,137,307.40 |
| Use of Goods and Service | 35 | 3,300,753,355.68 | 3,872,667,147.47 |
| Maintenance Expenses | 36 | 445,683,705.00 | 1,518,283,880.85 |
| Depreciation of Property, Plant and Equipment | 37 | 931,761,586.62 | 1,118,765,146.10 |
| Other Expenses | 52 | 37,104,896.00 | 51,104,219.13 |
| Social Benefits | 56 | 2,351,320,695.14 | 209,103,962.00 |
| **Total Expenses** | | **27,534,159,794.90** | **24,974,061,662.95** |
| Transfer | | | |
| Other Transfers | 60 | 190,694,846.29 | 221,883,483.55 |
| Total Transfer | | 190,694,846.29 | 221,883,483.55 |
| **TOTAL EXPENSES AND TRANSFERS** | | **27,724,854,641.19** | **25,195,945,146.50** |
| **Surplus** | | **5,782,046,295.06** | **7,329,261,686.65** |

**Hadija M. Kabojela**
**District Executive Director**
Date: 23/3/2024

**Hon. Gagi L. Gagi**
**Council Chairman**
Date: 23/3/2024

23 MAR 2024 — USHETU DISTRICT COUNCIL

Controller and Auditor General — AR/LGA/83/3118/2022/23

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT OFFICE -REGIONAL ADMINISTRATIVE AND LOCAL GOVERNMENT
00833118 - USHETU DISTRICT COUNCIL

### STATEMENT OF CHANGES IN NET ASSET AND EQUITY FOR THE PERIOD ENDED 30 JUNE 2023

| | Accum. Surplus/(Deficit) TZS | Other Reserve TZS | Total (TZS) |
|---|---|---|---|
| **Opening Balance as at 01 Jul 2022** | **21,547,880,991** | **36,000,000** | **21,583,880,990** |
| | - | | |
| Surplus/ Deficit for the Year | 5,782,046,295 | - | 5,782,046,295 |
| **Closing Balance as at 30 Jun 2023** | **27,329,927,286** | **36,000,000** | **27,365,927,286** |
| **Opening Balance as at 01 Jul 2021** | **12,272,061,097** | **76,032,700** | **12,348,093,797** |
| **Other Reserve** | (40,032,700) | (40,032,700) | (40,032,700) |
| Other Appropriations | 1,946,558,207 | - | 1,946,558,207 |
| Surplus/ Deficit for the Year | 7,329,261,686 | - | 7,329,261,687 |
| **Closing Balance as at 30 Jun 2022(Restated)** | **21,547,880,990** | **36,000,000** | **21,583,880,991** |

**Hadija M. Kabojela**
**District Executive Director**
Date: 23/3/2024

**Hon. Gagi L. Gagi**
**Council Chairman**
Date:

23 MAR 2024 — USHETU DISTRICT COUNCIL

Controller and Auditor General — AR/LGA/83/3118/2022/23

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT OFFICE -REGIONAL ADMINISTRATIVE AND LOCAL GOVERNMENT
00833118 - USHETU DISTRICT COUNCIL

### CASHFLOW STATEMENT FOR THE PERIOD ENDED 30 JUNE 2023

| | Note | 2023 (TZS) | Restated 2022 (TZS) |
|---|---|---|---|
| **CASH FLOW FROM OPERATING ACTIVITIES** | | | |
| **RECEIPTS** | | | |
| Subvention from other Government entities | 32 | 31,662,316,574 | 25,365,611,635 |
| Social Contributions (Revenue) | 20 | 206,384,668 | 266,192,788 |
| Revenue from Exchange Transactions | 17 | 1,459,105,316 | 836,383,970 |
| Other Revenue | 31 | 5,726,100 | 7,498,100 |
| Levies | 18 | 288,603,169 | 1,179,632,227 |
| Increase in Deposit | 94 | 233,780,432 | - |
| Fees, Fines, Penalties and Forfeits | 19 | 259,730,609 | 142,090,138 |
| Total Receipts | | 34,115,646,867 | 27,797,408,857 |
| **PAYMENTS** | | | |
| Wages, Salaries and Employee Benefits | 34 | 20,270,563,389 | 18,309,445,507 |
| Use of Goods and Service | 35 | 3,257,438,861 | 3,466,399,808 |
| Social Benefits | 56 | 2,351,320,695 | 209,103,962 |
| Other Transfers | 60 | 170,000,000 | 211,071,486 |
| Other Expenses | 52 | 37,104,896 | 51,104,219 |
| Maintenance Expenses | 36 | 445,683,705 | 1,518,283,881 |
| Decrease in Deposit | 94 | - | 46,312,323 |
| Total Payments | | 26,532,111,547 | 23,811,721,187 |
| **NET CASH FLOW FROM OPERATING ACTIVITIES** | | **7,583,535,320** | **3,985,687,671** |
| CASH FLOW FROM INVESTING ACTIVITIES | | | |
| Investing Activities | | | |
| Payment for Work in Progress | 82 | 2,738,306,965 | 2,091,871,379 |
| Acquisition of Property, Plant and Equipment | 77 | 3,430,195,884 | 3,728,510,991 |
| Total Investing Activities | | 6,168,502,850 | 5,820,382,370 |
| **NET CASH FLOW FROM INVESTING ACTIVITIES** | | 6,168,502,850 | 5,820,382,370 |
| **CASH FLOW FROM FINANCING ACTIVITIES** | | | |
| Financing Activities | | | |
| Cash proceeds from other short or long-term borrowings | 102 | 87,692,300 | (259,850,000) |
| Total Financing Activities | | 87,692,300 | (259,850,000) |
| **NET CASH FLOW FROM FINANCING ACTIVITIES** | | 87,692,300 | (259,850,000) |
| Net Increase | | 1,327,340,171 | (1,574,844,699) |
| Cash and cash equivalent at beginning of period | 62 | 579,337,943 | 2,154,182,643 |
| Cash and cash equivalent at end of period | | 1,906,678,114 | 579,337,943 |

**Hadija M. Kabojela**
**District Executive Director**
Date: 23/3/2024

**Hon. Gagi L.Gagi**
**Council Chairman**
Date: 23 MAR 2024

Controller and Auditor General — AR/LGA/83/3118/2022/23

### 1.0 INDEPENDENT REPORT OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL

Hon. Chairperson of the Council,
Ushetu District Council,
P.O. Box 50,
**Kahama, Shinyanga.**

### 1.1 REPORT ON THE AUDIT OF FINANCIAL STATEMENTS

**Unqualified Opinion**

I have audited the financial statements of Ushetu District Council, which comprise the statement of financial position as at 30 June 2023, the statement of financial performance, statement of changes in net assets, cash flow statement and the statement of comparison of budget and actual amounts for the year then ended, as well as the notes to the financial statements, including a summary of significant accounting policies.

In my opinion, the accompanying financial statements present fairly in all material respects, the financial position of Ushetu District Council as at 30 June 2023, and its financial performance and its cash flows for the year then ended in accordance with International Public Sector Accounting Standards (IPSAS) Accrual basis of accounting and the manner required by the Local Government Finances Act, Cap. 290.

**Basis for Opinion**

I conducted my audit in accordance with the International Standards of Supreme Audit Institutions (ISSAIs). My responsibilities under those standards are further described in the section below entitled "Responsibilities of the Controller and Auditor General for the Audit of the Financial Statements". I am independent of Ushetu District Council in accordance with the International Ethics Standards Board for Accountants' Code of Ethics for Professional Accountants (IESBA Code) together with the National Board of Accountants and Auditors (NBAA) Code of Ethics, and I have fulfilled my other ethical responsibilities in accordance with these requirements.

I believe that the audit evidence I have obtained is sufficient and appropriate to provide a basis for my opinion.

**Key Audit Matters**

Key audit matters are those matters that, in my professional judgment, were of most significance in my audit of the financial statements of the current period. I have determined that there are no key audit matters to communicate in my report.

**(iv) Procurement made outside of the E-procurement System - TZS 450,980,880**

I noted that, Ushetu District Council made procurement of building material, office consumables and other equipment worth TZS 450,980,880 outside the E-procurement System contrary to Reg.342 of the Public Procurement Regulations, 2013 and issued directive through Circular No.4 of 2019 by the Ministry of Finance.

### 1.2.2 Compliance with the Budget Act and other Budget Guidelines

**Subject matter: Budget formulation and execution**

I performed a compliance audit on budget formulation and execution of Ushetu District Council for the financial year 2022/23 as per the Budget Act and other Budget Guidelines.

**Conclusion**

Based on the audit work performed, I state that, except for the matters described below, Budget formulation and execution of Ushetu District Council is generally in compliance with the requirements of the Budget Act and other Budget Guidelines.

**(i) Non allocation of own source revenue to development activities - TZS 238,690,395**

I noted that, for the financial year 2022/23, the Council collected TZS 1,906,948,463 from its own sources of revenue in which the Council was required to allocate and utilize TZS 762,779,385 as 40% to development activities contrary to Paragraph 147 (E)(i) of the Guidelines for the Preparation of Annual Plan and Budget for 2022/23 requires Councils to allocate and contribute 40% of its own sources revenues collections to Development activities However, the Council allocated TZS 524,088,990 equivalent 69% leaving a balance of TZS 238,690,395 not contributed to developments.

**(ii) Implementation of projects not budgeted - TZS 4,622,790,690**

I noted that, the Council paid TZS 4,622,790,690 for construction of various projects at lower levels, for activities which were not budgeted. This is contrary to requirement of Section 46 (5) of the Local Government Finances Act, Cap. 290 [R.E 2019].

Charles E. Kichere
**Controller and Auditor General,**
**Dodoma, United Republic of Tanzania.**
**March 2024**

Controller and Auditor General — AR/LG/3118/2022/23

# Samia aipongeza NSSF mafanikio miaka mitatu ya uongozi wake

**Na Mwandishi Wetu,** KATAVI

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, ameupongeza Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) baada ya kuelezwa mafanikio mbalimbali katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake.

Alitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki alipotembelea banda la NSSF kwenye kilele cha Wiki ya Wazazi iliyofanyika Mjini Mpanda, mkoani Katavi. NSSF imeshiriki kutoa elimu ya hifadhi ya jamii katika maadhimisho hayo kwa kuwa Jumuiya ya Wazazi ni mojawapo ya wanachama.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma, Lulu Mengele, alisema alisema Mfuko huo unamshukuru Rais Samia kwa namna alivyofungua nchi, wafanyakazi kwenye sekta binafsi wakiwamo wa viwandani kuongezeka na kuiwezesha NSSF kupata wanachama wapya.

"Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan tunakupongeza kwa kazi kubwa unayoifanya, umefungua fursa mbalimbali ambapo wakati unaingia madarakani mwaka 2021 thamani ya NSSF ilikuwa ni Sh. trilioni 4.8, lakini sasa imepanda kwa juhudi kubwa ambazo umefanya tumefikia trilioni 8.5," alisema.

Aidha, NSSF inaendelea kuboresha mifumo yake ya TEHAMA na hivi sasa mwajiri anaweza kumwandikisha na kuwachangia wafanyakazi wake kulekule walipo na pia mwanachama anaweza kuangalia taarifa zake mbalimbali bila ya kulazimika kufika katika ofisi za NSSF na kwa hatua hiyo imerahisisha huduma kwa wanachama.

Akizungumzia ushiriki wa NSSF katika kilele cha Wiki ya Wazazi, Lulu alimweleza Rais Samia kuwa NSSF imeshiriki maonesho yaliyoandaliwa na Jumuiya ya Wazazi kwa kuwa wafanyakazi wa Jumuiya hiyo ni wanachama wake kama zilivyo Jumuiya nyingine za Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Lulu alisema wametumia maonesho hayo kutoa elimu ya hifadhi ya jamii kwa wanachama waliotembelea kwenye banda hilo, matumizi ya mifumo kwa waajiriwa na waajiri na wakiwa popote wanaweza wakapata taarifa zao za michango na kuwasilisha bila kulazimika kutembelea ofisi za NSSF.

Alisema NSSF inaendelea kufanya vizuri kwa kuweka kipaumbele cha kuwarahisishia huduma wanachama wake.




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akipata maelezo kutoka kwa Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma wa NSSF, Lulu Mengele, alipotembelea banda la NSSF katika kilele cha Wiki ya Wazazi iliyofanyika Mpanda mkoani Katavi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CWT: Kikokotoo cha mafao bado tatizo

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

BARAZA la Chama cha Walimu Mkoa wa Morogoro (CWT) limesema kikokotoo cha mafao kilichopandishwa kutoka asilimia 33 hadi 40 bado kina shida zinazoathiri ukokotoaji mafao ya wastaafu.

Limemwomba Rais Samia amwagize waziri mwenye dhamana aangalie kikokotoo hicho kwa kuwa bado kimeonekana kuwa na changamoto kutokana na kutumia domineta badala ya nyumereta.

Akisoma tamko kwa niaba ya baraza hilo baada ya kumaliza kikao hicho, Mwenyekiti wa CWT Mkoa wa Morogoro, Jumanne Nyakirang'ani, alisema ni muhimu waziri huyo mwenye dhamana kurudi kwenye kanuni ya 1/540 badala ya 1/580 (faida ya uwekezaji) ambayo inalalamikiwa pamoja na kanuni ya 15.5-15.5 (muda unaotarajiwa mstaafu kupokea mafao).

"Huo ni mfano rahisi tumeutoa kihesabu, hivyo tunamwomba waziri mwenye dhamana kurudi kwenye kanuni kwani bado kuna malalamiko kwa watumishi wastaafu kuhusu ukokotoaji," alisema Nyakirang'ani.

Mwenyekii huyo wa CWT alisema kuwa kwa muda mrefu watumishi wa umma walikuwa na kilio hicho bila ufumbuzi, lakini katika utawala wa Rais Samia wamepata ufumbuzi, jambo ambalo imewalazimu kutoa shukrani, hivyo waendelee kuboresha kikokotoo kwa siku zijazo ikibidi kirejeshwe kwenye asilimia 50 ya awali. Baraza hilo pia limepongeza hatua ya serikali kwa uamuzi wake wa kulipa madeni ya walimu ya mishahara na yasiyo ya mishahara kwa zaidi ya asilimia 71.

Nyakirang'ani alisema chama hicho kimekuwa na uhusiano mzuri na serikali kuanzia ngazi ya halmashauri, na kinapewa ushirikiano katika kushughulikia changamoto zinazohusu walimu.

Mmoja wa wajumbe wa baraza hilo kutoka Wilaya ya Kilosa, Richard Chagungu ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Wilaya ya Kilosa alisema Rais Samia amekuwa msikivu kwa kujali maslahi ya watumishi wa umma kwa kusikiliza kilio chao na kupandisha kikokotoo kilichokuwa kinalalamikiwa kwa muda mrefu.

Alimshauri Rais Samia kutokuchoka kuwasikiliza kwa kuwa wafanyakazi wanatamani afikie kwenye kikokotoo cha mstaafu kile cha awali cha asilimia 50 au aende juu zaidi ya hapo. Mwakilishi wa Walimu Vijana Mvomero, Ernestar Candidus, mwalimu wa Shule ya Msingi Mnyanza, alipongeza serikali kupandisha madaraja na kuboresha maslahi yao. Hatua hiyo imeongeza morali ya kazi.

Baraza la CWT katika ngazi ya mkoa linafanyika mara moja kwa mwaka kwa mujibu wa katiba ya chama hicho toleo la 6 la mwaka 2014, kifungu na.18.2 likiwashirikisha wajumbe 57.

# H'shauri Bagamoyo yapambania gati usafirishaji abiria Zanzibar

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Shauri Selenda, amesema anaendelea kupambania uwapo wa gati kwa ajili ya usafirishaji wa abiria kwenda Zanzibar ili kuinua uchumi kwa wakazi wa wilaya hiyo.

Selenda amesema wamefikisha maombi kwa wizara husika kuomba boti za kutoka Bagamoyo kwenda Zanzibar na anaamini suala hilo litashughulikiwa kwa muda mwafaka.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizindua mradi wa utunzaji wa rasilimali za baharini unaotekelezwa na Asasi ya BANGONET iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani.

Selenda alisema uwapo wa gati katika mji wa Bagamoyo utasaidia usafiri kwa wananchi hususani wanaojishughulisha na rasilimali za baharini kwenda Zanzibar na kurejea katika mji huo kufanya shughuli za biashara mbalimbali, pia itasaidia kuendelea kukua kwa mji huo.

Akizungumzia mradi huo, alisema asasi hiyo inatakiwa kuwashirikisha kikamilifu wananchi eneo la mradi ili waweze kutumia vizuri bahari kujiinua kiuchumi na kufanya mambo ya maendeleo.

"Serikali pekee haiwezi kufanya kila kitu ila kwa kushirikiana na wadau kama hizi asasi tunatasaidiana kuleta mabadiliko hasa katika mji wetu huu wa Bagamoyo wananchi waweze kutumia vizuri bahari kuleta mabadiliko kwenye maisha yao, kuna ufugaji wa majongoo bahari na mwani tutumie vizuri fursa tulizonazo," alisema. Kadhalika alisema kwa sasa serikali ipo katika sera ya uchumi wa buluu na suala la kutunza na kuendeleza rasilimali za bahari ni la kila mmoja kwa ajili ya maendeleo ya wananchi na utunzaji wa rasilimali hizo utaibua fursa ya ajira kwa vijana na pia elimu watakayopata itawawezesha kuwainua kiuchumi kwa kufuga kaa, majongoo bahari na kulima mwani pamoja kulinda mazalio ya samaki.

Mwenyekiti wa BANGONET, Maria Chidosa alisema asasi yao ina miradi mitano wameiandaa kwa utekelezaji mmoja wapo ukiwa ni wa uendelezaji wa rasilimali za bahari.

Alisema vikwazo wanavyokabiliana navyo kwa sasa ni pamoja na ukosefu wa fedha za kutekelezea miradi yako katika Wilaya ya Bagamoyo ambalo limechangiwa na ugonjwa wa UVIKO ndani na nje ya nchi.

Mratibu wa mradi huo kutoka BANGONET, Leonard Bankuwia, alibainisha mradi huo unalenga kujenga uwezo kwa jamii za wakazi wa maeneo ya ukanda wa Pwani ya Bagamoyo katika kutunza, kusimamia na kuendeleza rasilimali za bahari na kujiongezea vipato.

Bankuwia alisema katika utekelezaji wa mradi huo wanakusudia kujenga mahusiano na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kuwezesha upatikanaji wa boti za kisasa tatu hadi nne kwa ajili ya ulinzi wa doria baharini na kukomesha uvuvi haramu.

Pia shughuli zinakusudiwa kufanywa na asasi hiyo kwa kushirikiana na serikali, sekta za umma na binafsi, asasi za kiraia vyama vya wafanyabiashara na taasisi za kidini ambazo ni pamoja na kuendesha mikutano na wadau wanaotumia rasilimali za bahari, kuhakikisha vikundi vya usimamizi wa rasilimali za bahari (BMUs), vinakuwa na miradi ya kujiongezea kipato.

Mkakati mwingine ni kuandaa mchakato wa kuwapo kwa sheria ndogo za utunzaji, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za bahari kupitia Halmashauri ya Bagamoyo na Chalinze na pia kushawishi wakazi wa vijiji vya ukanda wa Pwani na kushawishi wa kurugenzi wa halmashauri hizo kutenga bajeti kwa ajili ya viongozi wa BMUs waweze kwenda kujifunza masuala ya utunzaji, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za bahari katika visiwa vya Zanzibar na Mombasa nchini Kenya.

Baadhi ya wadau walioshiriki katika mkutano huo Shumina Rashid ambaye ni Diwani Viti Maalumu wa Halmashauri ya Bagamoyo, alisema bado hali ya maeneo ya fukwe za bahari kwa ukanda wa wilaya hiyo ni chafu na kwamba asasi hiyo kwa kushirikiana na vikundi vya utunzaji wa rasilimali za bahari kujipanga kufanya usafi.

Mwinyi Hashim mkazi wa Kata ya Dunda, alisema ni vema ukawekwa utaratibu wa kupanda mikoko pembezoni mwa bahari kuzuia mmomonyoko, pia elimu kwa wavuvi inatakiwa kutolewa ili wawe makini na zana wanazotumia katika shughuli za uvuvi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kanuni kutaka wacheze wageni nane tu haikubaliki

**KUNA** taarifa kuwa moja kati ya mapendekezo ya kanuni zitakazoendesha Ligi Kuu msimu ujao, ni kuzuia wachezaji wote 12 wa kigeni kutocheza katika mechi moja, badala yake wadau wanapendekeza wawe wanane tu.

Katika kumbukumbu zetu, hii si kanuni mpya kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, kuna wakati ilishakuwapo, lakini ikalalamikiwa sana na wadau wa soka, wakiwamo makocha mbalimbali waliokuwa wakifundisha klabu nchini hasa wa Simba na Yanga.

Tunajua kuna mapendekezo ya kanuni bora kabisa ambazo zitaufanya mpira wetu kuendelea kupanda na kupendwa Afrika, lakini si hii ya kutaka wachezaji wanane wa kigeni ndiyo wacheze kwenye mechi moja.

Nadhani bado kuna wadau wa soka hawajatambua ni kwa nini soka la Tanzania kwa sasa limekuwa gumzo, limetokea kupenda Afrika, kiasi cha kuwa namba sita.

Haijafika hapo kwa bahati mbaya, ni kwamba imeruhusu wachezaji wa kigeni wacheze kwa kujinafasi na hiyo imezifanya timu za Simba na Yanga kufanya vema kwenye michuano ya kimataifa mfululizo kuliko wakati mwingine wowote katika historia ya soka la Tanzania.

Huwezi kuelezea mafanikio ya Simba kwa miaka mitano mfululizo au miwili ya Yanga bila kuwataja wachezaji wa kigeni kina Meddie Kagere, Haruna Niyonzima, Clatous Chama, Emmanuel Okwi, James Kotei, Sadio Kanoute, Djigui Diarra, Djuma Shaaban, Pacome Zouzoua, Maxi Nzengeli, Fiston Mayele, Stephane Aziz Ki na wengineo wengi waliokuwa wakiunda vikosi vya timu hizo.

Ukiwaondoa hao, sidhani kama Simba na Yanga zingeweza kufika hapo, kwani huko nyuma wakati zikitumia wazawa wengi, hata kuingia makundi tu Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho ilikuwa mtihani.

Ndiyo msimu uliomalizika Yanga wakiingia makundi Ligi ya Mabingwa mara ya kwanza tangu 1998 na Simba iliingia 2017/18, mara ya kwanza baada ya 2003.

Uwapo wa wachezaji wengi wa kigeni ndiyo umefanya hivi Tanzania iwe na nafasi nne za uwakilishi, lakini pia hata viongozi wa pande zote mbili wakiwa na uwezo wa kusimama mbele ya watu kusema wanataka ubingwa wa Afrika, wachezaji hao wamesababisha hata Timu ya Taifa ya Tanzania kwa sasa kuwa imara na kutoziogopa hata za mataifa ya nje yenye majina makubwa.

Hii ni kwa sababu wachezaji wengi wanacheza nao kwenye ligi au wapo timu moja. Hivyo kuwapunguza tunatengeneza nafasi nne za wachezaji ambao wana uhafadhali na si kiwango cha soka, hivyo hata wakichaguliwa Stars wanakwenda kwa sababu wanacheza mara kwa mara kwenye timu na wale si viwango vyao.

Tunaomba Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF) na Bodi ya Ligi nchini (TPLB), kutupilia mbali mapendekezo hayo kwani yataleta athari kubwa katika soka letu. Tunataka Mtanzania akipata namba, basi awe amewazidi viwango wageni ama analingana nao na si kwa kubebwa na kanuni, hapo ndipo tunatapowapata wachezaji wazuri kikosi cha Taifa Stars.

Kwa miaka hii michache ambapo hakuna kanuni za ajabu za kuwazuia wageni, wakiwa 12 na kocha ana uwezo wa kuwachezesha wote, ndipo tumeiona Stars bora zaidi, yenye wachezaji waliokomaa na kupambana kutokana na kukomazwa na wageni hao hao.

Kutowawekea kanuni ya upendeleo, kumewafanya wachezaji kwa ubora kama Ibrahim Hamad 'Bacca', Mudathir Yahaya, Dickson Job, Clement Mzize, Nickson Kibabage, kupigania namba na kuwaweka benchi wageni upande wa Yanga, Mohamed Hussein 'Tshabalala', Shomari Kapombe, Mzamiru Yassin, hata Ladack Chasambi na Edwin Balua kuonyesha makali yao wakiwa na timu ya Simba, huku kule Azam mchezaji Feisal Salum na Yahaya Zayid hata hawahitaji kanuni hiyo ili kupata nafasi Stars.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wachezaji Ligi Kuu msikimbie ushindani, pambanieni namba

Na Adam Fungamwango

**WAKATI** usajili wa wachezaji ukiendelea nchini, kuna taarifa kuwa baadhi ya wachezaji wanaondoka kwenye klabu wanazozichezea kwa kuhofia kupoteza namba.

Nimepenyezewa taarifa kuwa baadhi ya wachezaji wakiwamo hata wale ambao wanaichezea Timu ya Taifa, Taifa Stars au waliowahi kuichezea wanaondoka, wengine wakishinikiza kutaka kuondoka kutimkia timu nyingine ambako wanaamini watapata nafasi ya kucheza au hakuna ushindani mkubwa wa kugombea nafasi ya kuanza kikosi cha kwanza.

Hao ni wale ambao walikuwapo kwenye kikosi, lakini walipoona usajili wa wachezaji ambao wanadhani wanaweza kuwaletea changamoto, wao wanaona bora waondoke, lakini wapo ambao walikuwa wanashinikiza wenzao waondolewe ili wao wabaki, hii ni baada ya kuongezewa mikataba, wao wanaamua kuondoka.

Naweza kusema kuwa tabia hii ni ya kujishusha thamani kwa mchezaji mwenyewe na kutojiamini. Mimi ninavyojua moja ya tabia ya mchezaji soka wa ukweli ni kujiamini, kujiona anaweza kucheza popote pale, lakini pia kuwa na tabia ya kujitoa mhanga.

Mchezaji mpira mzuri ni yule ambaye ana uwezo wa kujitoa mhanga, au kuamia jambo gumu hata kama baadaye linaweza kumletea madhara. Mfano mdogo wapo wachezaji walioamua kuacha hata ajira jeshini ili kwenda kujiunga na Klabu za Simba na Yanga, ili mradi tu kuweka masharti ambayo yatafidia kile ambacho alikuwa akipate akiwa huko. Na wengi wamefanya hivyo na wamefanikiwa, ingawa katika hilo ni lazima wawepo ambao hawakufanikiwa sana.

Mchezaji anayeogopa changamoto ya mchezaji wenzake kwenye namba ni kujiona kuwa yu dhaifu na kukubali kuwa hana uwezo wowote, badala yake amefika pale kwa bahati mbaya.

Nitoe mifano tu ya wachezaji ambao hawakuogopa kwenda timu zenye wachezaji mahiri, au waliokuwapo hawakulazimisha kuondoka baada ya kuletewa wachezaji wengine.

Simba iliwahi kumchukua Daud Salum 'Bruce Lee' ili kucheza beki wa kulia, iliyokuwa na Shaaban Baraza, Fibert Lubibisa alisajiliwa kama beki wa kushoto wakati Mohamed Kajole 'Machela' yupo, Yanga ilikuwa na beki wa kati Allan Shomari, lakini ilimleta Ishaka Hassan, kwenye kiungo ya kukaba ilikuwa na Issa Athumani, baadaye ikamsajili Athumani China, hakuna wakati ambao aliyekuwapo akaomba kuondoka kwa kumhofia anayekuja, wala anayekuja kuogopa kujiunga na timu kwa kuhofia kutopata namba.

Ni kwa sababu wote wao waliamini uwezo wao, kila mmoja aliamini kuwa kujituma kwenye mazoezi ndiko kutasababisha kupata namba.

Na kweli, vikosi vingine vya zamani vilikuwa na wachezaji ambao wanaweza kucheza namba moja, lakini uwezo ukawa unalingana na huwezi kutofautisha.

Simba ikawa na makipa, Mohamed Mwameja, Steven Nemes na Joseph Katuba, wote wakiwa kwenye kikosi kwa msimu mmoja, wakiwa ni makipa wa Taifa Stars na wote walikuwa wakiitwa.

Yanga ilikuwa na Joseph Fungo na Hamisi Kinye, makipa wa viwango vya juu kabisa, hakuna aliyemkimbia mwenzake, Pamba ikiwa na Madata Lubigisa na Paul Rwechungura.

Hii yote ni mifano michache inayoonyesha kuwa changamoto huwa hazikimbiwi bali zinakabiliwa na njia ni kujituma na kufanya kazi kwa bidii tu.

Nadhani hata wale ambao wanafundisha vijana kwenye 'akademi', waanze kuwafundisha jinsi ya kuwa wavumilivu, kujituma na kutokata tamaa, kwani linaonekana ni jambo linaloanza kuwasumbua vijana wengi si kwenye soka tu, bali nyanja nyingi.

Vijana wengi wanapenda sehemu ambayo ni rahisi tu, hawapendi sana changamoto, ndiyo maana hupenda maisha ya raha na starehe na kutaka kupata vitu vingi vikubwa kwa muda mfupi bila kuvifanyia kazi ngumu.

Linapotokea jambo gumu kidogo ambalo linahitaji nguvu ya upambanaji, kujitoa au uvumilivu wanashindwa. Hiki ndicho kinachotokea kwenye soka wakati huu wa usajili. Mimi nawashauri wapambane ili kupata namba na si kukimbia, kwa sababu changamoto hazikimbiwi, bali inabidi kukabiliana nazo.

## HABARI KITAIFA

# SUMAJKT yaanika kilichoibeba ushindi maonesho ya Sabasaba

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT) limeibuka mshindi wa kwanza katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi kwenye Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (Sabasaba).

Kutokana na ushindi huo, uongozi wa shirika hilo umetumia fursa hiyo kualika wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza kwao.

Mkuu wa Chuo cha Uongozi Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Kanali Stanslaus Mishako, aliyemwakilisha Mkuu wa JKT na Ofisa Mtendaji Mkuu wa SUMAJKT, Meja Jenerali Rajabu Mabele, alikaribisha wawekezaji baada ya kutangazwa mshindi katika maonesho hayo yaliyofungwa juzi na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

"JKT jukumu lake ni malezi ya vijana, uzalishaji mali na ulinzi. Kwanini tumekuwa wa kwanza? Ni kwamba jukumu kubwa tulilonalo JKT ni malezi ya vijana ambayo yanakwenda sambamba na kuwafundisha mambo mbalimbali ambayo wakimaliza mafunzo wanajiajiri wenyewe.

"Mahali ambako unaweza kujiajiri kirahisi ni sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi. Kilimo ni uti wa mgongo, hata ukisikiliza mkazo wa serikali ni kuhamasisha vijana kujikusanya katika makundi ili wajiajiri katika kilimo," alisema.

Kanali Mishako alisema kupitia maonesho hayo, JKT imetoa elimu kwa jamii katika sekta hizo zilizowapa ushindi na ndicho pia hufanyika kambini.

"Tunaposema wekeza katika kesho iliyo bora, tunazingatia wananchi na vijana kupata elimu ambayo inahusiana na kilimo, uvuvi na mifugo.

"Ndio maana majaji walipokaa, waliona hilo kwa kuwa maonesho haya ni eneo la kuelimisha umma. Majaji wameridhia kwamba wataalamu tulionao ni wenye weledi wa kutoa elimu.

"Ushirikiano uliopo JKT, umahiri wa wataalamu wa sekta mbalimbali, zikiwamo ujenzi na biashara ni uthibitisho tosha kwa ushindi huu," alisema.

Alisema JKT wakifanikiwa katika nyanja ya chakula kwa kujitosheleza, wataondoa tatizo la uhaba na kuwa na uhakika wa chakula.

Alisema kama kaulimbiu inavyosema, "Tanzania ni Mahali Sahihi kwa Biashara", hivyo rai yao kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi waendelee kuwekeza kwao.

Mkurugenzi wa Huduma na Biashara, Luteni Kanali Dorah Kawawa, ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji SUMAJKT, Kanali Petro Ngata, akizungumzia kaulimbiu ya mwaka huu, alisema wao kama Shirika la Uzalishaji la Jeshi la Kujenga Taifa, wanaitekeleza kaulimbiu hiyo kwa kufanya biashara na uwekezaji.

Alisema kuwa na mashamba, mbuzi, ng'ombe, kondoo, kuku na kujishughulisha na ufugaji nyuki kumechangia kuwapa ushindi katika maonesho hayo.

Vilevile, alisema wanatekeleza majukumu yao katika sekta ya uzalishaji maji ya kunywa, viwanda vya ushonaji nguo na cha utengenezi bidhaa za ngozi na kingine wameingia ubia na China kinachozalisha taa zinazotumia mwanga wa jua.

Pia alisema wana sekta muhimu za huduma na biashara ambapo wanatoa huduma ya walinzi kwa kutumia teknolojia ya hali ya juu, na sasa wanaweza kuvuka mipaka kwa kuwa wamejitosheleza kwa kupata vyeti vya kimataifa kwa ajili ya kufanya biashara.

Kanali Mishako alisema wanafanya ukandarasi wa kujenga barabara na madaraja, wakiikita pia kuzalisha bidhaa bora katika kampuni kwa kuzingatia uhitaji wa soko na muda.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maonesho hayo katika banda la JKT, Meja Josephat Yongo, alisema, "Banda hili limetuwezesha kupata ushindi mkubwa kutokana na namna tunavyotekeleza sera za kilimo, uvuvi na ufugaji mkubwa. Sisi ni shamba darasa, tunafundisha namna ya kupata mazao katika eneo dogo.

"Hata ufugaji samaki tumefundisha waliotembelea banda letu kwamba unaweza kuwa na eneo dogo ukafuga kwa kufuata masharti unayopewa na wataalamu wetu," alisema.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo (kulia), akimkabidhi tuzo Mkuu wa Chuo cha Uongozi Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Kanali Stanslaus Mishako, aliyepokea kwa niaba ya Mkuu wa JKT na Ofisa Mtendaji Mkuu wa SUMAJKT, Meja Jenerali Rajabu Mabele, baada ya SUMAJKT kuwa mshindi wa kwanza katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi katika Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) juzi mkoani Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ulinzi kuimarishwa stesheni ya SGR

**Na Ashon Balaigwa,**
MOROGORO

UONGOZI wa Mkoa wa Morogoro kwa kushirikiana na Shirika la Reli (TRC) wameahidi kuimarisha ulinzi kwa abiria wanaotumia treni za umeme zinazofanya safari zake kati ya Morogoro na Dar es Salaam.

Wameonya wenye nia mbaya ya uhalifu wa aina yoyote wasithubutu kufanya hivyo, serikali ikitambua kwa kuwasajili na kuwapanga watoahuduma za usafiri na wasafirishaji wakiwamo madereva wa magari madogo ya biashara (taxi), bodaboda na bajaji pamoja na mamalishe nje ya Stesheni ya Morogoro.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, akiwa ameambatana na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama na uongozi wa TRC, aliyasema hayo wakati akikagua stesheni hiyo mwishoni mwa wiki kisha kuzungumza na watoahuduma hao.

Malima alisema Stesheni ya Morogoro kila siku inapokea na kusafirisha watu zaidi ya 1,000 wanaotumia treni hiyo, hivyo wameamua kuimarisha ulinzi na usalama kwa kuwatambua watoahuduma wote ili watoe huduma bora pasi na kuwapo vitendo vya uhalifu.

Mkuu wa Mkoa alitoa wiki mbili kwa uongozi wa Manispaa ya Morogoro kujenga na kukamilisha banda la kisasa kwa ajili ya matumizi ya wajasiriamali (mamalishe) karibu na kituo cha treni ya reli ya kisasa (SGR) eneo la Kihonda.

Alisema lengo ni kuwezesha kinamama hao kutoa huduma za vyakula, vinywaji na matunda katika mazingira bora na salama kwa abiria na wao wenyewe kujipatia kipato.

Ni agizo alilotoa baada ya kupokea ombi la wanawake wajasiriamali wapatao 32 waliokosa eneo la kufanyia biashara zao na kupanga bidhaa zao kando ya barabara ya magari inayoingia na kutoka katika kituo hicho, kinyume cha utaratibu uliowekwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC).

"Mkurugenzi wa Manispaa Morogoro ninakuagiza utengeneze eneo kwa ajili ya kinamama hawa wafanye biashara zao, wapate sehemu, hili lifanywe ndani ya wiki mbili na liwe tayari," aliagiza Malima.

Alisema eneo watakalotengewa liwe na huduma mbalimbali zikiwamo za maji, vyoo na sehemu ya kupumzika wateja wanaosubiri muda wa kupanda treni.

"Tengenezeni mchoro mzuri na ndani ya siku tatu mje na ubunifu na kuniambia, eneo hili ni lenu na wajasiriamali hawa ni wenu," aliagiza Malima. Mkuu wa Mkoa pia alionya wajasiriamali hao kuchukue fedha za mikopo na kwenda kuzitumia kwa malengo tofauti, akisisitiza mafanikio yao ni kioo kwa wanawake wengine.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Wajasiriamali Wanawake, Happiness Chilingo alishukuru Mkuu wa Mkoa kwa kuwapatia eneo la kufanyia biashara zao karibu na kituo hicho.

"Tulikaa hapa eneo ambalo hatutakiwi kufanya biashara na tulikuwa tunafukuzwa, tunamshukuru Mkuu wa Mkoa kwa ujio wake na tusikiliza kilio chetu na tumekubaliwa, sasa tunaandaliwa eneo," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Alex Mkama, alisema wasafirishaji abiria, maarufu bodaboda, wanapaswa kuwa na sifa zote za kisheria wanazolazimika kuwa nazo ili kuruhusiwa kubeba abiria wa treni ya mwendokasi katika Stesheni ya Morogoro, vinginevyo wataenguliwa.

Alizitaja sifa hizo ni pamoja na kuwa na leseni, kofia ngumu, usafi pamoja na kuhakikisha wamesajiliwa na uongozi wa umoja wa madereva wa eneo hilo.

Kamanda Mkama aliyasema hayo mara baada ya kukutana na madereva wa taxi, bajaji na bodaboda wanaobeba abiria wa treni ya mwendokasi katika Stesheni ya Morogoro.

Stesheni ya Morogoro hivi sasa inapokea na kusafirisha abiria mara nane kwa siku, hivyo kuwa na idadi ya wasafiri kuwa kubwa huku walio wengi wakitegemea usafiri wa taxi, bajaji na bodaboda kuwafikisha kituoni hapo au kuwapeleka makwao pindi wakiwasili Morogoro.

Kamanda Mkama alisema Jeshi la Polisi Mkoa wa Morogoro limeimarisha ulinzi katika maeneo yote ya kituo hicho na hakuna tukio lolote la kihalifu liliwahi kuripotiwa tangu kuanza kwa usafiri huo.

Gidion Temu, bodaboda anayefanya shughuli zake katika kituo hicho, alishukuru Jeshi la Polisi kwa kuweka utaratibu huo na kuahidi kufuata sheria.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# UCHUMI COMMERCIAL BANK LTD

CARING FOR FAMILY ECONOMY

## GHARAMA ZA HUDUMA KUFIKIA TAREHE 30.06.2024

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| A | **DEPOSIT RATES** | **Descriptions** | **RATES(USD) - Products** | **RATES(TZS) - Products** |
| | Savings Account **(p.a)** | | | 1% |
| | Mavuno Account - Special Deposit Account (p.a) | | | 9% |
| | **Fixed Deposit** | | | |
| | 3 Months | | | 4% |
| | 6months | | | 5% |
| | 12Months | | | 6% |
| | Negotiable rates for Amount Exceeding 50Mil | | | 6% to 7% |
| | Negotiable rates for Amount Exceeding 100Mil | | | 8% to 9% |
| | Negotiable rates for Amount Exceeding 500Mil | | | 10% |
| B | **CHARGES AND FEES** | | | |
| | **ITEM/TRANSACTION** | | | CHARGE/FEE |
| 1 | **Current Accounts** | | | |
| | Minimum Opening balance - Company and individual | | 50.00 | 100,000.00 |
| | Minimum Operating Balance | | | - |
| | Monthly Statement enquiry | | 2.00 | TZS 1,500 per month and TZS 700 for extra page |
| | Monthly Ledger fee | | 5.00 | 15,000.00 |
| | Account closing charges | | 10.00 | 20,000.00 |
| | Sale of bankers cheque | | | 30,000.00 |
| | Cancelation of bankers cheque | | | 30,000.00 |
| | Cheque book per leaf | | 0.18 | 400.00 |
| | Stop payment order | | 10.00 | 30,000 reported lost/stolen cheque book/leaf (per notice) |
| | Standing order within the bank per entry | | 2.00 | 2,000.00 |
| | Standing order to other banks per entry | | 20.00 | 15,000.00 |
| | Confirmation of Balance and Audit statement | | 25.00 | 50,000.00 |
| | Salary processing fee per entry | | N/A | 2,000.00 |
| | Upaid cheque (RD) | | 40 | 40,000.00 |
| | Montly fees - Parishes Account | | N/A | 5,000.00 |
| | - Other Current Account | | N/A | 15,000.00 |
| | Quartely fees - Other Current account | | 5 | 2,000.00 |
| | Current Accounts - Individual withdrawal over counter | | 5 | 2,000.00 |
| | Current Accounts - Individual monthly fees | | 5 | 5,000.00 |
| | Current Accounts - SACCOS withdrawal over counter | | | 2,000.00 |
| | Deposit fee | | | free |
| | Withdrawal on current account using cheque | | | |
| | | 1 - 399,999 | | 1,500.00 |
| | | 400,000 - 4,999,999 | | 1,800.00 |
| | | 5,000,0000 - 9,999,999 | | 2,000.00 |
| | | 10,000,000 and above | | 0.05% |
| | Withdrawal on current account without cheque | Any Amount | | 5,000.00 |
| 2 | **Savings Accounts** | | | |
| | Minimum Operating Balance | Mavuno Saving Account | | 5,000.00 |
| | | Personal Saving | 10 | 10,000.00 |
| | | Other Savings Products | | 10,000.00 |
| | Account closure | | 10 | 20,000.00 |
| | Dormant account reactivation | | | free |
| | Withdrawal fee over the counter- Savings Products | | 1% of the withdraw amount | |
| | | 1 - 399,999 | | 1,500.00 |
| | | 400,000 - 4,999,999 | | 1,800.00 |
| | | 5,000,0000 - 9,999,999 | | 2,000.00 |
| | | 10,000,000 and above | | 0.05% |
| | Account maintenance fee - Monthly - Saving products | | | 1,500.00 |
| | - Quartely - Saving products | | | 1,600.00 |
| | Bulk Cash deposit | | | free |
| | New ATM card issuance | N/A | | 10,000.00 |
| | ATM card renewal or replacement | N/A | | 15,000.00 |
| | ATM withdrawal fee | 1,000 - 99,999 | | 1,500.00 |
| | | 100,000 - 400,000 | | 1,700.00 |
| | PIN Reset ATM | | | 5,000.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3 | **Electronic Banking** | | | |
| | SWIFT/TISS transfer | 1 - 9,999,999 | | 2,000.00 |
| | | 10,000,000 - 50,000,000 | | 5,000.00 |
| | | 50,000,000.1 and above | | 10,000.00 |
| | Mobile banking balance enquiry | | | 200.00 |
| | Transfer from bank account to mobile - As per TIPS schedule below | | | |
| | Mobile - PIN reset | | | 2,000.00 |
| | **Other Charges** | | | |
| | Cheque clearing fee (Outward Cheques) | | | 1,000.00 |
| | EFT | | | 2,000.00 |
| | Search fees (including vouchers) | one Month | | Free |
| | | Two(2) to six(6) month | 10 | 20,000 |
| | | Above six(6) month | 25 | 50,000 |
| | | CCTV footage Maximamu of 3 months | Tzs equivalent | 30,000 |
| | | | | |
| | Uncollected cheque book (after notification) | | | TZS 2,000 per month |
| | Coins deposit | Percentage of deposit amount for non parish | | 3% |
| | Brela Search Fees | Company Limited | | TZS 25,000 |
| | | Trade name | | TZS 7,000 |
| 4 | **Internet Banking** | | | |
| | 24/7 Transfer UCB to UCB | | | Free |
| | 24/7 Transfer (Other Banks) | | | 11,800.00 |
| | 24/7 Fund transfer (Bank to Mobile) - as per TIPS schedule below | | | |
| | 24/7 Airtime processing | | | free |
| | 24/7 Government payment | | | free |
| | 24/7 Other payments (utility) | DSTV, Star Times, AZAM, Subsciption services, bettings, Air tickets etc. | | 1,500.00 |
| | Balance inquiry | | | Free |
| | Monthly fee per retail user | | | 1,500.00 |
| | Monthly fee for corporate user | | | 2,500.00 |
| | Retail & Corporate subsricption | | | Free |
| | Bank statement self download | | | 500.00 |
| | Cheque book request 100 leaves | | | 47,200.00 |
| | Cheque book request 50 leaves | | | 23,600.00 |
| | PIN Regeneration | | | Free |
| | Salary processing | | | 500.00 |
| | Standing Order Instructions | | | 2,000.00 |
| | TIPS | 1 - 49 999 | N/A | 1,400.00 |
| | | 50,000 - 99 999 | N/A | 2,000.00 |
| | | 100,000 - 299,999 | N/A | 3,000.00 |
| | | 300,000 - 999,999 | N/A | 4,500.00 |
| | | 1,000,000 - 1,999,999 | N/A | 6,500.00 |
| | | 2,000,000 - 2,999,999 | N/A | 8,500.00 |
| | | 3,000,000 - Above | N/A | 10,500.00 |
| 5 | **Agency Banking** | | | |
| | Agent Cash withdraw charges | 1,000-29,999 | N/A | 1,500.00 |
| | | 30,000-49,999 | N/A | 1,500.00 |
| | | 50,000-99,999 | N/A | 1,500.00 |
| | | 100,000-299,999 | N/A | 1,600.00 |
| | | 300,000-499,999 | N/A | 3,200.00 |
| | | 500,000-999,999 | N/A | 3,250.00 |
| | | 1,000,000-1,999,999 | N/A | 4,450.00 |
| | | 2,000,000-2,999,999 | N/A | 6,550.00 |
| | | 3,000,000-3,999,999 | N/A | 7,650.00 |
| | | 4,000,000-4,999,999 | N/A | 8,750.00 |
| | | 5,000,000-5,999,999 | N/A | 9,850.00 |
| | Agent cash deposit | | | Free |
| | Agency Banking - Balance enquary | | | 500.00 |

**UCB OFFERS THE FOLLOWING PRODUCTS:**

CARING FOR FAMILY ECONOMY

- *Savings Accounts*
- *Current Account*
- *Elimu Juniour Account*
- *Mavuno Savings Account*
- *Uchumi Savings Account*
- *Fixed Deposit Accounts-(FDR) with attractive Rates*
- *Forex Accounts*
- *Bureau De Change*
- *ATMs Services, all over the Country-Umoja Switch*


# TIRA yataka nguvu zaidi Bima ya Afya kwa Wote

**Na Restuta James**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bima (TIRA) imezielekeza kampuni za bima nchini kuweka mkazo wa kutoa huduma ya bima ya afya nafuu kwa wananchi ili Watanzania wengi wanufaike pale wanapougua.

Maelekezo hayo yalitolewa juzi na Kamishna wa Bima, Dk. Baghayo Saqware, alipozungumza na waandishi wa habari kwenye Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam, maarufu Sabasaba.

"Tumeelekeza kampuni za bima zitoe bidhaa na huduma rahisi, nafuu na rahisi kupatikana. Ndio maana unaona hata sisi tumesajili utoaji bima kidijitali.

"Tunawasihi wananchi watumie huduma na bidhaa za bima kwa sababu kwa kufanya hivyo unaweza kujiondolea umasikini kwa urahisi hasa unapopatwa na janga," alisema.

Kamishna huyo alisema TIRA imepanua wigo wa kupata huduma hizo kwa kusajili benki na bima mtandao kuuza bima ili wananchi wahudumiwe kwa urahisi.

Dk. Saqware alisema kwa wastani sekta hiyo inakua kwa asilimia 15 na kwamba wananchi wengi wanakata bima za mali kama vile magari.

Hata hivyo, alisema watu wameanza kuelewa umuhimu wa bima ya maisha ambayo ni kinga na uwekezaji kwa mnufaika.

"Bima ya maisha inakua sana lakini kwa idadi ya watu. Kwa mfano, mwaka 2022, tulikuwa na watu milioni sita wanaotumia huduma za bima, mwaka jana waliongezeka hadi watumiaji milioni 12. Walioongezeka zaidi ni watu wa bima ya maisha ambao hata hivyo idadi yao ni ndogo kulinganisha na wanaonunua bima za mali," alisema.

Alitaka wananchi kuchangamkia bima ya maisha ili wajikinge na pia wawekeze katika kampuni mbalimbali na kupata faida.

Katika hatua nyingine, Kamishna Saqware alisema katika kipindi chote cha Sabasaba, zaidi ya wananchi 5,000 walipewa elimu ya bima. "Tunapenda kutoa rai kwa wananchi kwamba waendelee kutumia huduma za bima. Bima ni kinga kwa mali, afya na uwekezaji. Ni huduma inayokuondolea umasikini kwa kuhakikisha unarudi salama pale unapokumbwa na janga," alisema. Alisema kwa sasa sekta ya bima inachangia asilimia 1.99 ya Pato la Taifa na lengo ni kutoa mchango wa asilimia tatu ifikapo mwaka 2030.

Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ilipitishwa na Bunge Novemba Mosi mwaka jana na kutiwa saini na Rais Samia Suluhu Hassan Novemba 19, 2023.





Meneja wa Wakala wa Barabara mkoani Manyara, Dutu Masele (katikati) na viongozi wengine wakifuatilia kikao cha bodi ya barabara cha mkoa huo kilichofanyika mjini Babati juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanaohusika na ulinzi wa taarifa watakiwa kujisajili

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKURUGENZI Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Emmanuel Mkilia, ameziagiza taasisi zinazohusika na ulinzi wa taarifa binafsi kutoka kwa watoa huduma wa simu na benki wasiokamilisha usajili wahakikishe wanajisajili kabla ya Desemba mwaka huu.

Alitoa agizo hilo jana jijini Arusha wakati akifunga mafunzo ya ulinzi wa taarifa binafsi kwa maofisa wa ulinzi wa taarifa binafsi (DPO's) kwa wakusanyaji na wachakataji wa taarifa kutoka benki na kampuni za simu.

Alisema usajili ni hatua muhimu katika kuhakikisha kwamba kila mmoja anatambuliwa na kuidhinishwa kufanya kazi katika ulinzi wa taarifa binafsi. Alisema vizuri wakumbuke kwamba jukumu la kulinda taarifa binafsi ni zito na linahitaji umakini na tahadhari ya hali ya juu. Aidha, aliwataka watumie mafunzo hayo, kwa vitendo na kuwa mabalozi bora wa ulinzi wa taarifa binafsi.

Alisema lengo la mafunzo hayo ya siku nne ni kuwajengea uwezo katika kulinda taarifa binafsi za watu na kuhakikisha usalama wa mifumo ya taarifa.

Vile vile aliwaomba wajenge nidhamu katika kutekeleza majukumu yao ya kulinda taarifa binafsi ni nzito na linahitaji umakini na tahadhari ya hali ya juu, kwa kufuata miongozo, taratibu na kanuni zilizowekwa, ili kufanya kazi zao kwa ufanisi na kwa uaminifu. Hivyo, aliwasihi wawe na nidhamu, uadilifu na weledi katika kazi zao ili kuhakikisha kuwa taasisi za kifedha na watoa huduma za mawasiliano ya simu zinakuwa salama na za kuaminika kwa wateja wao.

Alisema wanapaswa kuwa waangalifu na makini katika kudhibiti upatikanaji wa taarifa hizo, ili kuepuka matumizi mabaya au wizi wa taarifa.

# KKKT yawasilisha hoja 3 za watu wenye ulemavu NHIF

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KITENGO maalum cha kujenga uwezo na kulea jamii ya wenye ulemavu (BCC) cha Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), kimewasilisha mambo matatu katika Ofisi ya Rais (TAMISEMI), kikitafuta ufumbuzi wa changamoto ya wenye ulemavu kushindwa kulipa vifurushi vilivyoainishwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Wadau hao, wanaiomba serikali iongeze kifurushi maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu ili kutimiza mpango wa usawa katika huduma za afya kwa watu wenye ulemavu, yaani afya kwa wote.

Mratibu wa BCC, Elirehema Kaaya, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taifa wa Mtandao wa Tanzania Community Basic Rehabilitation Network (CBR), aliwasilisha mapendekezo yao jana kwa Mkurugenzi wa Huduma za Jamii, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), anayeshughulikia makundi maalum, Amina Mfaki.

Mfaki alikwenda katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, kuzungumza na watoto wenye ulemavu wa akili na viungo waliokuwa wakishiriki bonanza la 'BCC Disability Festival' lililotanguliwa na kauli mbiu, 'Sote ni wa jamii moja, furaha yetu ni ya thamani kuliko hali zetu.'

"Kwa hiyo ombi kwa serikali ni kutupatia PT (Physiotherapist) au OT (Occupational Therapist-wataalamu wa mazoezi tiba) angalau wanne. Mmoja katika kila jimbo Hai, Karatu, Kilimanjaro Mashariki na Siha.

Alisema pili, kuna suala la wenye ulemavu kushindwa kumudu gharama za matibabu na dawa kwa watu wenye ulemavu na familia zao.

Aidha, alisema kumekuwa na changamoto ya kushindwa kulipa vifurushi vilivyoainishwa na NHIF.

"Tunaiomba serikali iongeze kifurushi maalum, kwa kuwa makundi haya yanaitwa makundi maalum, basi kuwapo na umaalumu huo pia, kwa ajili ya watu wenye ulemavu ili kutimiza mpango wa usawa katika huduma za afya kwa watu wenye ulemavu, yaani afya kwa wote.

"Na jambo la tatu, ni ukosefu wa ajira kwa watu wenye ulemavu. Ziko jitihada kubwa zimefanywa na mashirika ya kuwezesha vijana wenye ulemavu kujitambua na kuelimika; na sasa wapo baadhi yao, wana uwezo wa kufanya kazi katika jamii.

...Tunaiomba serikali na taasisi binafsi, kutoa fursa zaidi za ajira kwa vijana hawa ili waweze kujikimu kimaisha."

Akijibu ombi la wadau hao, Mkurugenzi huyo wa TAMISEMI, Mfaki, alisema serikali inauona upunguful huo, lakini kila mwaka imekuwa ikiajiri watumishi.

Akitolea mfano alisema walimu vijana wenye ulemavu walioajiriwa kwa mwaka 2020/22/23, walikuwa 110, wakati kwa upande wa afya, vijana wenye ulemavu ambao hawakufichwa wakaenda wakasoma kada ya afya, wameajiriwa 96.

"Mwaka 2021/22 asilimia zaidi ya mbili ya watumishi waliokuwa wameomba ajira walikuwa ni wenye ulemavu. Hivyo, nakubaliana kwenye suala la ajira, serikali na sekta binafsi, sote tuone namna gani tunawajengea uwezo wanafunzi kozi mbalimbali na kuajiriwa au wajiajiri," alisema.

Kuhusu gharama kubwa za bima ya afya, Mfaki alisema: "Utoaji wa huduma za afya unaongozwa na Sera ya Afya ya Mwaka 2007. Sera hii sehemu ya tano, kipengele kidogo, 1.1.3, kimeeleza msamaha wa gharama za uchangiaji wa huduma za afya kwa makundi maalum.

...Hivyo serikali inatambua uwepo wa wananchi wasio na uwezo, ikiwamo watu wenye ulemavu na tunaamini kuwa watu wenye ulemavu siyo wote ambao hawana uwezo.

"Kuna watu wenye ulemavu ambao wanaweza kumudu maisha yao vizuri kabisa. Lakini kwa wale ambao wana changamoto ya kimaisha, uwezo mdogo sera hii ya afya imewatambua kwamba watatibiwa bila malipo."

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo wa TAMISEMI, kwa mwaka 2022/23, watu wasio na uwezo, wakiwamo wazee zaidi ya 500,000 wametibiwa bila malipo, kwa gharama ya Sh. bilioni mbili zililipwa na serikali.

Kuhusu watu wenye ulemavu kuongezewa vifurushi vya bima ya afya ili kusaidia usawa katika utoaji wa huduma, alisema jambo hilo lipo na linatambulika.

# Sillo ataka ushirikiano wananchi, serikali vita ukatili

**Na Allan Isack,** BABATI

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani, Daniel Sillo, amesema katika suala la mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia ikiwamo ubakaji na ulawiti wanavyofanyiwa watoto na wanawake katika jamii, wananchi wanapaswa kushirikiana na serikali kupiga vita matukio hayo.

Sillo ambaye ni Mbunge wa Babati Vijijini mkoani Manyara, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wa jimbo lake kwenye eneo la Kata ya Dareda wilayani Babati mkoani Manyara.

Hata hivyo, alisema jamii inapaswa kuendelea kushirikiana kwa karibu na serikali hususani vyombo vya usalama kwa kutoa taarifa mapema endapo watabaini viashiria vyovyote ili kudhibiti matukio hayo.

"Hakuna utajiri au mali zinazopatikana kwa njia ya kufanya ukatili, hivyo niwasihi ndugu zangu wananchi wa Dareda na Watanzania wenzangu, kwa ujumla kufanya kazi kwa bidii na ambayo haivunji sheria na utaratibu wa nchi kwa kuwa utajiri wa halali na wa amani unapatikana kwa kufanya kazi tu na si vinginevyo," alisema.








# 'Elimu kilimo biashara bado tatizo kwa wakulima'

**Na Gwamaka Alipipi**

MKURUGENZI wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'I Issa, amesema licha ya vijana wengi kujiajiri katika kilimo bado wengi wao hawana ujuzi wa kufanya kilimo biashara, hali inayowasababisha kubaki katika umaskini.

Amesema kutokana na hali hiyo kuna haja ya kuwaongezea ujuzi wakulima ili waondokane na kilimo cha mazoea na kukifanya kuwa cha biashara ili kiwakwamue kiuchumi.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, wakati akizindua Mtandao wa Kimataifa wa Kilimo Biashara (AMEA), unaoziunganisha nchi zaidi ya 80 duniani, kwa kutoa utaalamu wa kilimo biashara kwa wakulima wadogo.

"Wengi tunafahamu kwamba asilimia 67 ya Watanzania wamejiajiri katika kilimo. Lakini licha ya idadi hiyo wengi wao hawajui kufanya kilimo cha biashara hali inayowasababisha kuendelea kuwa maskini zaidi," alisema Beng'i.

Alisema takwimu zinaonyesha eneo la uingizwaji biashara katika kilimo linachangia pato la taifa chini ya asilimia mbili na hiyo ni kwa sababu Watanzania hawana ufahamu wa utalaamu wa biashara.

Alisema NEEC linashirikiana na AMEA kama mkono wa serikali kuhakikisha wakulima wanafanikiwa na kupewa mbinu bora za kujikwamua kutoka katika umaskini.

Beng'I alisema: "Tunajua kwamba Watanzania wengi wamejiajiri katika kilimo, kwa hiyo kama kilimo kitafanywa kwa tija tunaweza kufanya vizuri na kuchangia katika pato la taifa.

Mtandao huu wa AMEA unatuunganisha na mataifa mengine kwa lengo la kuwawezesha Watanzania kufaidika na huduma za ushauri na biashara, hivyo wakulima wetu wafanye kilimo biashara".

Mkurugenzi Mtendaji wa Jukwaa Huru la Kilimo (Ansaf), Honest Mseri, alisema endapo kutakuwa na jitihada za kuviimarisha vyama vya kilimo kutasaidia kuwapa mbinu bora wakulima za kujinasua kutoka katika umaskini.

Alisema lengo la kuingia katika AMEA ni kusaidia kilimo biashara kiwainue wakulima kiuchumi.

"Kwa sasa kuna mazao ya mboga na matunda ambayo yanapelekwa kwa wingi nje ya nchi, lakini kinachoangaliwa ni ubora, kwa hiyo tunatakiwa kuangalia huo ubora kwa wakulima ili waweze kuuza kwa wingi mazao nje ya nchi," alisema na kuongeza:

Naye Mkurungenzi wa AMEA duniani, Mark Blackett, alisema mtandao huo upo kwa ajili ya kusaidia mitandao ya wakulima pamoja na kutoa mbinu bora za kilimo.



Canara Bank (Tanzania) Ltd.

(Together we can build a better life)

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA WA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2024

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 30 Juni 2024 | Robo Mwaka iliopita 31 Machi 2024 |
|---|---|---|---|
| A | **MALI** | | |
| | 1 Fedha Taslimu | 486.11 | 396.39 |
| | 2 Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 3,928.41 | 7,082.37 |
| | 3 Uwekezaji katika Amana za serikali | 34,930.89 | 38,183.73 |
| | 4 Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 546.79 | 401.75 |
| | 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | (12.20) | (13.38) |
| | 6 Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| | 7 Bili zilizoafikiwa | - | - |
| | 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| | 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 9,249.55 | 1,522.40 |
| | 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| | 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 41,861.81 | 43,090.28 |
| | 12 Mali Nyingine | 1,909.89 | 1,740.43 |
| | 13 Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| | 14 Akaunti za udhamini | - | - |
| | 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,343.37 | 1,087.53 |
| | 16 **JUMLA YA MALI** | **94,244.61** | **93,491.50** |
| B | **DHIMA** | | |
| | 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | 771.00 |
| | 18 Amana za Wateja | 50,177.65 | 48,532.45 |
| | 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | 20 Amana Maalumu | - | - |
| | 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| | 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| | 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,571.15 | 1,480.30 |
| | 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| | 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| | 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| | 27 Dhima Nyingine | 378.06 | 705.93 |
| | 28 Madeni | - | - |
| | 29 **JUMLA YA DHIMA** | **52,126.87** | **51,489.68** |
| | 30 **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29* | **42,117.75** | **42,001.83** |
| C | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| | 32 Akiba ya Mtaji | 157.47 | 230.53 |
| | 33 Mapato Yaliyobakizwa | 8,320.13 | 8,247.06 |
| | 34 Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 810.15 | 694.23 |
| | 35 Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| | 36 Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| | 37 **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **42,117.75** | **42,001.83** |
| | 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 5,475.59 | 4,288.42 |
| | 39 Mikopo Chechefu | 306.11 | 410.12 |
| | 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 66.26 | 75.68 |
| | 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 44.69% | 44.93% |
| | (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.73% | 0.95% |
| | (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 83.54% | 87.54% |
| | (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 44.42% | 46.09% |
| | (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 91.88% | 88.99% |
| | (vi) Ongezeko la Amana | 1.77% | -15.11% |
| | (vii) Ongezeko la Mali | 0.81% | -8.52% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 JUNI 2024

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 30 Juni 2024 | Robo ya mwaka linganishi (mwaka uliopita) 30 Juni 2023 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30 Juni 2024 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30 Juni 2023 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 2,114.76 | 2,120.77 | 4,513.15 | 4,234.02 |
| 2 Gharama za Riba | 585.33 | 791.75 | 1,196.47 | 1,595.61 |
| 3 **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,529.43** | **1,329.02** | **3,316.68** | **2,638.41** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 51.51 | - | 53.16 | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 7.42 | 113.27 | (95.03) | 123.75 |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba** | **64.09** | **94.51** | **209.27** | **301.78** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 5.01 | 34.70 | 53.04 | 82.93 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 59.08 | 59.80 | 156.23 | 218.86 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **1,268.67** | **1,018.64** | **2,457.67** | **1,961.41** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 513.81 | 374.59 | 993.85 | 797.35 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 10.55 | 5.71 | 13.70 | 11.57 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 744.32 | 638.33 | 1,450.12 | 1,152.48 |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **265.92** | **291.62** | **1,110.15** | **855.04** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 150.00 | 155.00 | 300.00 | 440.00 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **115.92** | **136.62** | **810.15** | **415.04** |
| 11 Idadi ya Waajiriwa | 26 | 24 | 26 | 24 |
| 12 Mapato kwa Hisa | 4 | 4 | 25 | 13 |
| 13 Mapato kwa Hisa | 4 | 4 | 25 | 13 |
| 14 **Idadi ya Matawi** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.49% | 0.51% | 1.72% | 0.77% |
| (II) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1.10% | 1.33% | 3.87% | 2.03% |
| (III) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 79.61% | 71.56% | 69.70% | 66.71% |
| (IV) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 7.18% | 5.40% | 7.78% | 5.30% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 JUNI 2024

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 30 Juni 2024 | Robo Mwaka iliopita 31 Machi 2024 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30 Juni 2024 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30 Juni 2023 |
|---|---|---|---|---|
| **I Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 115.92 | 694.23 | 810.15 | 136.62 |
| Marekebisho kwa ajili ya: | - | - | - | - |
| Hasara katika mali | 209.04 | 85.05 | 294.09 | 96.03 |
| -Badiliko halisi katika Mikopo | 1,228.47 | 3,682.45 | 4,910.92 | 2,591.13 |
| Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika Amana | 874.20 | (8,774.87) | (7,900.67) | (3,789.20) |
| Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 51.18 | (494.11) | (442.94) | (11.26) |
| Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | 350.59 | 258.91 | 609.50 | (526.65) |
| Kodi iliyolipwa | (150.00) | (150.00) | (300.00) | (155.00) |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **2,679.39** | **(4,698.34)** | **(2,018.95)** | **(1,658.32)** |
| **II Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | | - | |
| Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za kudumu | (464.89) | (348.38) | (813.27) | (1.54) |
| Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | 3,240.59 | 6,442.89 | 9,683.47 | (1,988.09) |
| Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **2,775.70** | **6,094.51** | **8,870.21** | **(1,989.63)** |
| **III Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | (138.37) | 0.00 | (138.37) | (66.32) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **(138.37)** | **0.00** | **(138.37)** | **(66.32)** |
| **IV Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | | | |
| Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 5,316.72 | 1,396.17 | 6,712.89 | (3,714.26) |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka/mwaka | 12,355.14 | 10,958.97 | 10,958.97 | 17,337.24 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/mwaka** | **17,671.86** | **12,355.14** | **17,671.86** | **13,622.97** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2024

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 30/06/2024** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **32,830.00** | **-** | **8,216.29** | **261.30** | **-** | **-** | **41,307.59** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 810.15 | - | - | - | **810.15** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 103.83 | (103.83) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa Robo mwaka wa sasa** | **32,830.00** | **-** | **9,130.28** | **157.47** | **-** | **-** | **42,117.75** |
| **Mwaka Uliopita 31/12/2023** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **7,344.16** | **467.69** | **-** | **-** | **40,641.86** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 829.89 | - | - | - | **829.89** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (164.15) | - | - | - | **(164.15)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 206.39 | (206.39) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **8,216.29** | **261.30** | **-** | **-** | **41,307.59** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2024

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha,sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita(kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka sasa,mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| RAJSHEKHAR SOMASHETTY | OFISA MTENDAJI MKUU | (Imesainiwa) | 12-07-2024 |
| FADHILI PETRO SANGA | MKUU WA FEDHA | (Imesainiwa) | 12-07-2024 |
| FREDRICK HIPPOLITE | MKAGUZI MKUU WA NDANI | (Imesainiwa) | 12-07-2024 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi..**

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| INDIAEL DANIEL KAAYA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 12-07-2024 |
| MWANAIDI ATHUMAN MTANDA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 12-07-2024 |

**Canara Bank (T) Ltd**
**Head Office Dar Es Salaam Branch**
**Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania**
**E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532**
**www.canarabank.co.tz**



# Babu asakwa madai kumwozesha mjukuu

**Na Shaban Njia,** KISHAPU

MWANAFUNZI wa darasa la nne (jina limehifadhiwa (12) katika Shule ya Msingi Seseko wilayani Kishapu mkoani Shinyanga anadaiwa kukatishwa masomo na babu yake, Masangu Mahewa (65), kuozeshwa kwa mahari ya ng'ombe 16.

Inaelezwa kuwa mtoto huyo aliachishwa masomo miaka miwili iliyopita baada ya baba yake kufariki na mama yake kufukuzwa ukweni kwa madai kuhusishwa na kifo cha mume wake kwa njia za ushirikina, hivyo kumlazimu yeye (mtoto) kuishi na babu yake.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Kijiji cha Seseko, Kalonga Mwandu alikiri kupata taarifa za mwanafunzi huyo kuozeshwa na kusema alipofuatilia ili kujua undani wa suala hilo alisema mtuhumiwa alitoroka.

Alisema mzee huyo ametelekeza mifugo aliyopewa kama mahali nyumbani kwake na kuwa taarifa zinaonyesha mwanafunzi huyo aliozeshwa Kijiji cha Sengerema Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu.

Mkazi wa kijiji hicho, Samweli Jafari alisema matukio ya wanafunzi na mabinti chini ya miaka 18 kuozeshwa kwa kubadilisha na mifugo yapo mengi.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kennedy Mgani, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema bado wanaendelea na uchunguzi ili kuwabaini wahusika.

"Tumefika nyumbani kwa Msangu ambako tumekuta mifugo mbalimbali ikiwamo ng'ombe ambazo zinadaiwa kutolewa kama mahari, watuhumiwa wote akiwamo mwanafunzi wamekimbia na sasa tunaendelea na upelelezi," alisema Kamanda Mgani.

# Balozi aanika mikakati kukuza Kiswahili Burundi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BALOZI wa Tanzania nchini Burundi, Gelasius Byakanwa, amesema katika kuhakikisha lugha ya Kiswahili inafundishwa na kutumika katika nchi za Afrika Mashariki, nchi hiyo imeanza mikakati mahusus kufanikisha hiyo.

Balozi Byakanwa alitoa kauli hiyo juzi jijini hapa alipoambatana na wanafunzi na walimu wa vyuo vikuu kutoka Bujumbura nchini Burundi, lengo likiwa ni kutembelea miradi mbalimbali.

Alisema katika utekelezaji huo kama ubalozi waliamua kuikuza na kuisambaza lugha ya Kiswahili ikiwa ni pamoja na kuanzisha utaratibu wa kushindanisha wanafunzi wa vyuo vikuu katika uandishi wa insha mjini Bujumbura, lengo likiwa ni kuhakikisha wanakikuza na kukiendeleza nchini humo.

Aidha, alisema mikakati hiyo inalenga kutambua miongoni mwa juhudi zinazofanywa na serikali ya Tanzania katika kuhakikisha inaeneza Kiswahili sanifu katika nchi za Afrika Mashariki.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda alisema Tanzania itaendelea kushirikiana na Burundi katika sekta mbalimbali, huku akiwataka vijana hao kuhakikisha wanalinda amani waliyonayo.

Kadhalika aliwataka wanafunzi na walimu hao kuhakikisha wanaendelea kudumisha umoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuidumisha na kuiendeleza lugha ya Kiswahili ili iweze kukidhi vigezo vya kutumika katika nyanja nzima ya teknolojia.

# Nipashe Spotika



WACHEZAJI WENYE ASILI YA AFRIKA WALIOWIKA EURO 2024 UK. 12-13



# YAMAL NA NCHI TATU ZILIZOMGOMBEA

**ISIKUPITE**

HISPANIA na Ujerumani ndizo zilizoshinda taji la michuano ya Euro mara nyingi zaidi (kila moja mara tatu) zikifuatiwa na Ufaransa na Italia ambazo zimeutwaa ubingwa huo mara mbili kila moja. Hivyo Hispania jana ilikuwa ikiwania kuweka rekodi ya kuwa taifa la kwanza lililotwaa ubingwa huo mara nyingi zaidi tangu michuano hiyo ilipoanzishwa mwaka 1960, wakati England ilikuwa ikisaka nafasi ya kuubeba kwa mara ya kwanza.

**BERLIN,** Ujerumani

MCHEZO bora Lamine Yamal katika Mashindano ya Ulaya (Euro 2024), yaliyomalizika jana, Jumapili nchini Ujerumani, yanatazamiwa kukuza soka nchini Equatorial Guinea, linasema shirikisho la soka nchini humo.

Kijana huyo mwenye umri wa miaka 17, ambaye ameushangaza ulimwengu kwa weledi wake nchini Ujerumani, anaichezea Hispania licha ya kuwa na mama wa Equatorial Guinea na baba kutoka Morocco.

Alizaliwa Barcelona, ambako alikulia na kupitia akademi ya La Masia kwa mabingwa hao mara tano wa Ulaya, ambako hivi karibuni alihitimisha msimu wake wa kwanza wa kucheza.

"Ingawa Lamine haichezei Equatorial Guinea, tunamshikilia kwa karibu sana mioyoni mwetu na tunadhani atafanya mambo mengi kwa soka la Equatorial Guinea," anasema Venancio Tomas Ndong Micha, rais wa shirikisho la soka nchini humo, akiiambia BBC Sport Africa.

"Tunafurahia uchezaji wake wa ajabu kwenye michuano ya Euro, kando na msimu mzuri akiwa na FC Barcelona. Ana mizizi yetu, na hii inaonesha kuwa sisi ni nchi ya wanasoka wazuri," aliongeza Ndong Micha.

Akiwa amepewa fursa katika mechi kali ya taifa kubwa la kandanda barani Ulaya licha ya umri wake mdogo, Yamal ameonesha uwezo wake wa kila kitu kwa bao lake la kushangaza dhidi ya Ufaransa na kusaidia katika mechi dhidi ya Croatia, Georgia na Ujerumani.

Alicheza fainali dhidi ya England jana Jumapili, siku moja baada ya kufikisha umri wa miaka 17, na kumfanya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kutinga fainali kwenye michuano ya Euro au Kombe la Dunia.

Pele ndiye mwenye umri mdogo zaidi kucheza Fainali ya Kombe la Dunia. Alikuwa na miaka 17 siku 249 alipocheza katika ushindi wa Brazil wa 5-2 dhidi ya Sweden katika fainali ya 1958, alipofunga mara mbili.

Rekodi ya Yamal kama mfungaji mabao mdogo zaidi kwenye Euro (umri wa miaka 16 siku 361) itakuwa ngumu sana kuvunjwa. Vile vile mafanikio yake akiwa Barcelona - ambaye ndiye mchezaji mdogo zaidi kuanza mchezo wa ligi (miaka 16 na siku 38) - na katika La Liga, ambapo ndiye mfungaji mwenye umri mdogo zaidi katika historia (miaka 16 na siku 87).

## Hasahau mizizi yake

Equatorial Guinea ni nchi iliyogawanyika katika sehemu mbili, na Mji Mkuu wa Malabo uko kwenye moja ya maeneo ya visiwa vyake wakati mji mkubwa zaidi kwenye sehemu yake ya bara la Afrika ni Bata, ambapo mama yake Yamal alizaliwa.

Hatimaye alipata njia ya kwenda Hispania ambako alikuwa akifanya kazi kama mhudumu wa hoteli alipokutana na baba yake.

Wakati mama yake na nyanya yake wanaishi Barcelona, familia nyingine ya kinamama Yamal bado wako Equatorial Guinea, nchi ambayo imefika hatua ya mtoano katika michuano miwili iliyopita ya Kombe la Mataifa ya Afrika licha ya udogo wake.

Miaka mitatu iliyopita, Shirikisho la Soka la Equatorial Guinea (Feguifoot) lilijaribu kupata huduma ya winga huyo kwa timu hiyo ambayo kwa sasa inashika nafasi ya 89 kwenye orodha ya ubora ya Fifa, na kugundua walikuwa nyuma sana ya Hispania.

"Tuliwasiliana na familia mnamo 2021, lakini hatua na Shirikisho la Kandanda la Hispania ilikuwa mbele yetu," Ndong Micha alielezea.

"Lakini tulijaribu, kwa sababu mimi ni rafiki mzuri wa familia hiyo - haswa babu yake - na familia yote ilikuwa ikizungumza juu ya mtoto huyo.

"Kisha, pia kulikuwa na Waworocco ambao walimfuata ... lakini Wahispania walitushinda."

Faouzi Lekjaa, rais wa Shirikisho la Kandanda la Morocco, ameeleza jinsi majaribio yao ya kumpata Yamal mwaka jana yalivyoishia kushindwa, kutokana na nia thabiti ya kijana huyo kuichezea Hispania. Hata hivyo, nchi zote mbili za Kiafrika zinasalia kuwa karibu na moyo wa Yamal - kama inavyoonekana kwa uwapo wa bendera zao za kitaifa kwenye viatu vyake.

"Hii inaonyesha kwamba ingawa anaichezea Hispania, hasahau asili yake ya Equatoguinean," aliongeza Ndong Micha.

Ndong Micha anaamini kwamba Yamal analiweka taifa la mamake kwa uthabiti katika uangalizi wa kimataifa, akisema inalingana na mafanikio ya Ansu Fati katika umri mdogo, pia katika Barcelona, wakati watu walipojua kuhusu nchi ya familia yake ya Guinea-Bissau.

"Uchezaji wake - pamoja na ule wa kikosi cha kwanza cha Barca - unaonesha kwamba Equatorial Guinea ina njia tofauti sana ya kucheza ikilinganishwa na nchi nyingi za Afrika," anasema Ndong Micha.

"Kwa kuzingatia kipaji chake, na mizizi yake, siku moja tunaweza kuwa na wachezaji zaidi kama Lamine hapa."

Yamal si mchezaji wa kwanza mwenye asili ya Hispania mwenye asili ya Equatorial Guinea kugonga vichwa vya habari mwaka huu, baada ya Emilio Nsue kuwashangaza waangalizi wa kimataifa alipomaliza kama mfungaji bora katika Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka huu akiwa na umri wa miaka 34. Vichwa vya habari vya kimataifa vilifuatiwa mwezi uliopita, pale Fifa ilipoamua kuwa mshambuliaji huyo hajawahi kutangazwa kuwa anastahili kuichezea nchini hiyo ambayo ni mfungaji bora akiwa na mabao 22.

Hata hivyo, mabao yake yalisaidia kufika hatua ya 16. Taifa hilo la watu chini ya milioni mbili limefikia hatua ya mtoano katika Afcon zote nne walizoshiriki.

"Tunapaswa kuendelea kujiandaa vema," anasema Ndong Micha.

"Serikali hivi karibuni itawekeza katika akademi za soka ili tuweze kuibua Lamines na Emilios zaidi siku zijazo. Imejiandaa kuendelea kuwekeza kama ilivyofanya miaka ya hivi karibuni kuendelea kusaka vipaji vya asili kutoka Guinea ya Ikweta, lakini hasa katika nchi yenyewe.

"Kabla ya kuwasili kwangu, hatukuwahi kufuzu kwa Kombe la Mataifa kwa kufuzu kwetu - tulifuzu tu kama taifa mwenyeji (mara mbili) - lakini sasa tumefuzu mara mbili Afcon moja kwa moja (mwaka 2021 na 2023).

"Katika ngazi ya michezo, tukiwa na Fifa, Shirikisho la Soka Afrika, na serikali yetu tutaendelea kukua kisoka ili miaka michache ijayo, Equatorial Guinea iwe mfano wa nchi ndogo, lakini inayoweza kuziangamiza nchi kubwa kisoka"

Iwapo Ndong Micha atafanikisha matamanio yake na taifa hilo dogo la Afrika ya Kati likapata kufuzu kwa mara ya kwanza kwa Kombe la Dunia la kihistoria, kuna nafasi hata kwamba Yamal anaweza kukabiliana na taifa la mama yake kwenye hatua kubwa zaidi siku moja.

# WACHEZAJI WENYE ASILI YA AFRIKA WALIOWIKA EURO 2024



SAKA

**BERLIN,** Ujerumani

MASHINDANO ya Euro 2024 jana, Jumapili yalifikia tamati kwa England kucheza na Hispania kwenye mechi ya fainali.

Kwenye michuano hiyo, vijana wadogo wameonesha uwezo mkubwa, wengine wakiwa na asili ya Afrika.

**Tangu mashindano yaanze, baadhi ya wachezaji wenye asili ya Afrika wanafanya vema. Wachezaji hao wangekuwa na uwezo wa kucheza baadhi ya nchi barani Afrika.**

Hawa ni baadhi ya wachezaji waliofanya vizuri kwenye michuano hiyo wenye asili ya Afrika...

**Jamal Musiala**

Jamal Musiala kutoka Klabu ya Bayern Munich, alizaliwa Ujerumani. Ni kiungo mshambuliaji mwenye umri wa miaka 21, tayari yuko kwenye chati ya wafungaji mabao akiwa amecheka na nyavu mara tatu kabla ya mchezo wa jana. Ni mmoja wa wachezaji muhimu wa Ujerumani.

Musiala ana asili pana sana. Angeweza kuichezea England, Nigeria au Poland. Baba yake ana asili ya Nigeria na England, na Mama yake ni Mjerumani mwenye asili ya Poland.

**Lamine Yamal**

Winga wa Barcelona amepata umaarufu baada ya Kocha Xavi Xernandez kumpa nafasi ya kuchezea timu ya wakubwa.

Yamal amekuwa aking'ara katika klabu yake na hadi timu ya taifa akiwa na miaka 17 tu.

Katika msimu wa 2023/24, amecheza michezo 50 kwa Barcelona katika mashindano yote. Katika michuano ya Euro, winga huyo alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu wa Kocha wa Hispania, Luis de la Fuente.

Kijana huyo amekuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kucheza mechi ya Euro pamoja na kuwa mchezaji mdogo zaidi kufunga katika michuano hiyo.

Yamal angeweza kuichezea Morocco au Equatorial Guinea, asili ya wazazi wake - lakini amechagua Hispania alikozaliwa.

**Nico Williams**

Nico Williams ni ndugu wa mchezaji wa Athletic Bilbao na mshambuliaji wa Black Stars, Inaki Williams ambaye aliamua kuichezea Ghana Agosti 2022.

Lakini Nico ambaye alistahili kuichezea Ghana, aliamua kuichezea Hispania kutokana na kuzaliwa huko.

Nico akitafakari safari ya wazazi wake kutoka Ghana hadi Hispania anasema, "namshukuru Mungu kwamba tuko pamoja sasa na maisha ni mazuri. Wazazi wangu wanatazama watoto wao waking'ara - kila kitu tunachofanya ni kwa ajili ya wazazi wetu."

Katika michuano ya Euro, Nico ni mmoja wa wachezaji bora wa Hispania.

Tetesi zimeibuka kwamba Barcelona wanataka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21.

**Kylian Mbappe**

Baba yake Mbappe ni kutoka Cameroon na mama yake ana asili ya Algeria.

Mbappe mshambulizi wa zamani wa PSG ni mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani, na ana mizizi barani Afrika.

Mnamo Julai 2023, alipotembelea Yaounde, alisema: "Ni heshima kuwa pamoja na familia yangu na kuonana na marafiki wote ambao wanaonesha upendo mwingi," Mpabbe aliwaambia wanahabari.

"Nina mipango na miradi mingi kwa ajili ya Cameroon kwa watoto na kwa siku zijazo."

Mbappe aliyejiunga na Real Madrid amefunga bao moja na ametoa pasi moja iliosababisha bao kwenye michuano hiyo ya Euro 2024.

**Kwadwo Antwi Duah**

Kwadwo aliifungia Uswisi dhidi ya Hungary katika mchezo wa ufunguzi. Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 27, anaichezea Klabu ya Ludogoretz ya Bulgaria.

Alizaliwa London na wazazi kutoka Ghana mwaka 1997. Ni mmoja wa wachezaji watatu waliofunga kwenye mechi ya kwanza katika Timu ya Taifa ya Uswisi.

Baada ya mchezo huo alisema: "Huu ni mchezo wangu wa pili wa kimataifa, na nimefunga bao langu la kwanza - ninafuraha sana."

Katika majira ya kiangazi ya 2022, alipokea mwaliko kutoka Chama cha Soka cha Ghana kucheza mechi za mchujo za Kombe la Dunia la 2022 dhidi ya Nigeria, lakini alikataa ofa hiyo.

**Breel Embolo**

Embolo anaichezea Monaco, aliifungia Uswisi bao la tatu katika ushindi wa 3-1 dhidi ya Hungary.

Familia ya Embolo ni asili ya Cameroon. Katika Kombe la Dunia la 2022, Embolo hakusherehekea baada ya kufunga bao dhidi ya Cameroon.

Tangu alipocheza kwa mara ya kwanza 2015, sasa amecheza mechi 60 kwa Uswisi.

Embolo mwenye umri wa miaka 27, anaitembelea Cameroon kwa ajili ya likizo na pia familia na marafiki.

**Manuel Obafemi Akanji**

Akanji ana mama wa Uswisi na baba kutoka Nigeria. Baba yake pia alicheza mpira.

Akanji alisema, "Nchini Nigeria, nataka kuwasaidia watoto ambao hawajapata bahati kama niliyo nayo mimi nchini Uswisi."

Mlinzi huyo wa Manchester City, anasema Burna Boy ndiye msanii anayempenda zaidi. Ni mchezaji muhimu wa Timu ya Taifa ya Uswisi.

**Bukayo Saka**

Alizaliwa na wazazi kutoka Nigeria. Winga wa Arsenal anaiwakilisha England katika ngazi ya vijana na timu kubwa pia.

Shirikisho la Soka la Nigeria halijajaribu kumleta Saka, lakini haiwezekani kufanya hivyo baada ya kucheza katika Timu ya Vijana nchini England.

Saka amefanya vema ndani ya Arsenal msimu uliopita.

**Jeremy Frimpong**

Jeremy Frimpong ni mmoja wa wachezaji muhimu wa Bayer Leverkusen, iliyoshinda taji la Bundesliga akiwa na mabao nane msimu uliopita.

Ana umri wa miaka 23, amecheza michezo 31 katika klabu yake kabla ya Kocha wa Uholanzi, Ronald Koeman, kumwita kwa ajili ya Euro.

Chama cha Soka cha Ghana kilimwita Frimpong, lakini alikataa mwaliko wa kuichezea Ghana.

"Kocha wa Ghana alinipigia simu mwaka 2023, lakini nia yangu ni kuichezea Uholanzi," alisema Frimpong .

## Nukuu

"Mimi si muumini wa hadithi za hadithi bali ni muumini wa ndoto. Tumekuwa na ndoto kubwa na tumehisi umuhimu wa hilo, lakini lazima ufanye mambo hayo yatimie," **Kocha wa England, Gareth Southgate, kabla ya mchezo wa fainali ya Euro 2024 dhidi ya Hispania jana usiku.**



"Namshukuru Mungu kwamba tuko pamoja sasa na maisha ni mazuri. Wazazi wangu wanatazama watoto wao waking'ara – kila kitu tunachofanya ni kwa ajili ya wazazi wetu," **Nico Williams, aliyekinukisha na Hispania kwenye michuano ya Euro 2024, wazazi wake wakiwa na asili ya Ghana.**



"Je, hufikirii kuwa tayari ameweka historia ya kutosha, kwa kile alichokifanya hadi sasa? Anataka kutengeneza historia zaidi, tulifanya kila tulilolweza pamoja naye, pamoja na wafanyakazi wa matibabu, ili kumfanya awe hapa. Wakati wa maandalizi, alikuwa na tatizo kidogo la mgongo," **Kocha wa Ufaransa, Didier Deschamps, akimtetea nahodha wake, Kylian Mbappe, baada ya kukosolewa kutokana na uchezaji wa mshambuliaji huyo kwenye michuano ya Euro 2024 iliyomalizika jana.**





Kikosi cha Pyramids kikiwa na straika wao hatari, Fiston Mayele, ambacho kitavaana na JKU ya Zanzibar hatua za awali na huenda kikakutana na Azam FC, kama kitaitoa APR. **PICHA: MTANDAO**

# ZIJUE TAKWIMU ZA WAPINZANI SIMBA, YANGA, AZAM FC CAF

**Na Adam Fungamwango**

WIKI hii, Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), liliendesha droo na kutoa ratiba ya michuano linayoisimamia, Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho.

**Katika droo hiyo iliyochezeshwa Cairo nchini Misri, Yanga imepangwa kucheza dhidi ya Vital'O ya Burundi, huku Azam FC ikiangukia kwa APR ya Rwanda katika michezo ya Ligi ya Mabingwa Afrika, huku Mabingwa wa Zanzibar, JKU wakipangwa dhidi ya Pyramids ya Misri.**

Coastal Union ambayo ipo Kombe la Shirikisho Afrika itacheza dhidi ya Bravos do Maquis ya Angola, huku Simba itakayoanzia moja kwa moja raundi ya kwanza mwezi Septemba dhidi ya mshindi wa mechi ya awali kati ya mwakilishi kutoka nchini Libya na Uhamiaji kutoka Zanzibar.

Katika makala haya tunakuletea historia, takwimu na rekodi za timu ambazo ni wapinzani wa Simba, Yanga, Azam, JKU na Coastal Union.

**1. Vital'O**

Itakuwa nyumbani kati ya Agosti 16 na 18 kupambana na Mabingwa wa Tanzania Bara, Yanga kwenye mechi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Wenyewe ni Mabingwa wa Burundi, wakiwa wamemaliza ligi wakivuna pointi 72 katika mechi 30 walizocheza, ambapo ligi yao ina timu 16 kama ilivyo nchini.

Ilimaliza ikiwa imeshinda mechi 22, sare sita, ikipoteza mara mbili, ikipachika mabao 52 na kuruhusu 11.

Itacheza na Yanga, ambayo nayo kwenye ligi yake yenye timu 16, imevuna pointi 80, ikicheza mechi 30, kushinda 26, sare mbili na kupoteza mbili, ikipachika mabao 71 na kuruhusu wavu wake kuguswa mara 14.

Vital'O, iliyoanzishwa mwaka 1957, iliamua kujiita jina hilo 1975, baada ya kupitia majina kadhaa kama Gwanda, Sport FC miaka ya 1960, na kuanzia 1971, ikaitwa Atletico, baadaye ikabadilishwa na kuitwa Tout Puissant Bata mwaka 1973, jina ambalo halikukaa sana, ikajipachika tena jina la Espoir FC, ambalo nalo waliona halifai na hatimaye 1975, wakajiita Vital'O ambalo limeishi hadi leo.

Timu hiyo imetwa ubingwa wa nchi mara 20, Kombe la Burundi ambalo ni kama FA Cup kwa hapa nchini, mara 14.

Imetwaa Ubingwa wa Afrika Mashariki na Kati, maarufu kama, Kombe la Kagame mara tatu, huku mafanikio yao makubwa kwenye michuano ya kimataifa ni kufika hatua ya fainali ya Kombe la Washindi barani Afrika (sasa Kombe la Shirikisho Afrika), 1992 na kufungwa jumla ya mabao 5-1 dhidi ya African Sports ya Ivory Coast, ikitoka sare ya bao 1-1 nyumbani na kukong'otwa mabao 4-0 ugenini.

**2. APR FC**

Kwa sasa ipo nchini Tanzania, ikishiriki michuano ya Kombe la Dar Port Kagame, inayoendelea kwenye viwanja vya KMC, Mwenge, Dar es Salaam na Azam Complex, Chamazi.

Timu hii inayomilikiwa na Jeshi la Rwanda, jina lake kamili ni Armee Patriotique Rwandaise, na kila herufi ya mwanzo ya maneno hayo, ndiyo unapata jina la APR.

Itakumbana na Azam FC, katika mchezo wa awali wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Azam ikianzia nyumbani kati ya Agosti 16 na 18, marudiano yatafanyika Kigali, nchini Rwanda kati ya tarehe 23, mpaka 25 mwezi huo, kusaka timu itakayokwenda raundi ya kwanza ya michuano hiyo.

Ndiyo mabingwa wa nchi hiyo kwa sasa, wakiutwaa kwa kukusanya pointi 68, ambapo kwa michezo 30 iliyocheza, ilishinda 19, sare 11 na haikupoteza mechi yoyote ile katika ligi hiyo iliyokuwa na timu 16.

Itacheza na Azam ambayo yenyewe ilimaliza Ligi Kuu Bara ikiwa katika nafasi ya pili na pointi 69.

Imetwaa ubingwa wa Ligi Kuu mara 22, na Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini Rwanda, mara 13.

Kama itatwaa Kombe la Kagame mwaka huu basi itakuwa mara ya nne, kwani imeshawahi kufanya hivyo, mwaka 2004, 2007 na 2010.

Haijawahi kuingia kwenye makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika tangu ianzishwe mwaka 1993, lakini mafanikio yao makubwa kwenye michuano ya kimataifa ni kufika hatua ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika mwaka 2003, ilipotolewa na Julius Berger ya Nigeria, kwa jumla ya mabao 3-2, ambapo ilibamizwa mabao 3-0 ugenini, na kushindwa kusonga mbele licha ya kushinda mabao 2-0 nyumbani mechi ya marudiano.

**3. Pyramids FC**

Ni moja kati ya timu bora kwa sasa barani Afrika ambayo kwa sasa inaongoza Ligi Kuu nchini Misri ikiwa na pointi 68, ikiwa imecheza mechi 28, ikishinda 21, sare tano na kupoteza mbili, ikifuatiwa na Al Ahly ambayo ina pointi 60, lakini ikiwa imecheza michezo 24.

Itacheza na Mabingwa wa Zanzibar, JKU, ambayo imemaliza ligi msimu uliopita ikikusanya pointi 66 kwa michezo 30 iliyocheza.

Ikumbukwe kuwa mshindi wa mechi hii ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ndiye atakayecheza dhidi ya mshindi kati ya Azam FC dhidi ya APR ya Rwanda.

Pyramids ilianzishwa 2008 ikijulikana kama Al Assiouty Sport, kabla ya kubadilisha jina baadaye. Haijawahi kutwaa ubingwa wa Misri, lakini ilimaliza nafasi ya pili misimu ya 2018/19 na 2021/22, mshindi wa pili ya makombe ya FA, 2018/19 na 2021/22 na Super Cup ya nchini hiyo 2022/23.

Mafanikio yake makubwa zaidi mechi za kimataifa ni kufika hatua ya fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu wa 2019/20 ilipofungwa bao 1-0 dhidi ya RS Berkane ya Morocco katika mechi ya mkondo mmoja tu, iliyochezwa nchini Morocco.

**4. Bravos do Maquis**

Ni timu ngeni kwa masikio ya mashabiki wa soka nchini Tanzania. Inatoka nchini Angola ambapo itacheza dhidi ya Coastal Union kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, kuania Agosti 16 hadi 18, nyumbani, kabla ya kuwafuata wapinzani wao nchini Tanzania katika mechi ya marudiano.

Imemaliza nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu nchini Angola ikiwa na timu 14, ikicheza mechi 28, ikivuna pointi 37.

Bravos do Maquis ilianzishwa 1983, haina mafanikio yoyote kimataifa, wala nchini kwao, ambapo mwaka 2015 ilitwaa Kombe la FA, na mwaka unaofuata ikafika fainali ya Super Cup. Itachezwa na Coastal Union iliyomaliza Ligi Kuu ikiwa nafasi ya nne ikiwa na pointi 43.

**5. Uhamiaji/ Libya**

Simba ndiyo timu pekee itakayocheza mechi yake ya kwanza Septemba mwaka huu kwani haitocheza kwenye raundi ya awali, kutokana na kuwa ndani ya timu 10 bora za Afrika.

Katika droo iliyopangwa, itacheza moja kwa moja raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika na mshindi kati ya Uhamiaji ya Zanzibar na timu moja kutoka nchini Libya, ambako ligi hiyo inaendelea.

Kutokana na msimamo wa ligi nchini humo ilivyo, timu tano ambazo zinatarajiwa kucheza dhidi Uhamiaji ya Zanzibar na mshindi wake atapambana na Simba ni Al Ahly Tripoli, Al Nasr, Al Hilal Benghazi, Al Ahly Benghazi, na Al Madina.

Uhamiaji ni timu iliyoshika nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar iliyomalizika, ikikusanya pointi 47 katika michezo 30 iliyocheza.

Uhamiaji imepata nafasi ya kuiwakilisha Zanzibar katika michuano hiyo baada ya Chipukizi FC, timu iliyokuwa imefuzu kucheza kujiondoa kutokana na ukata.

**JE, WAJUA?**

-CONMEBOL- COPA AMERICA USA 2024

USHINDI kwa Argentina dhidi ya Colombia kwenye mchezo wa fainali ya Copa America utakaopigwa Miami, Marekani leo, utaifanya kuweka rekodi ya kushinda michuano hiyo mara nyingi zaidi (mara 16) moja zaidi ya Uruguay, tangu mashindano hayo yalipoanzishwa mwaka 1916.

# Kaya 20 zalalamika kupokwa maeneo

**Na Paul Mabeja,** BAHI

WANANCHI kutoka kaya 20 katika Kijiji cha Nkulugano wilayani Bahi mkoani Dodoma, walioporwa hekari zaidi ya 100 na serikali ya kijiji wamelalamika kukamatwa kila wanapohoji hatima ya maeneo yao yaliyochukuliwa kwa ajili ya ujenzi wa shule ya msingi na sekondari.

Pia wamelalamikia kitendo cha serikali ya wilaya kuwapiga marufuku kuingia katika maeneo hayo, ambayo baadhi yana makaburi ya ndugu zao na kushindwa kuyafanyia usafi.

Wakizungumza na waandishi wa habari, mmoja wa wakazi hao Bosco Ilunga, alisema mgogoro huo wa ardhi baina ya familia hizo na serikali umedumu kwa miaka zaidi ya 30 hali ambayo imewalazimu kuzunguka huku na huku bila mafanikio.

Ilunga alisema mgogoro huo ulianza mwaka 1993, ambapo serikali ya kijiji kwa kushirikiana na ya wilaya walichukua maeneo yao kwa nguvu kwa madai kuwa wanataka kupanua eneo kwa ajili ya ujenzi wa shule ya msingi na sekondari.

"Kweli hapo awali shule walituomba eneo kwa ajili ya kupanua eneo lao tukawapatia lakini sasa wamekuja tena kuongeza mpaka na kuingia katika mashamba yetu ambayo tunayatumia kwa ajili ya kilimo na shughuli nyingine za uzalishaji mali," alisema.

Hivyo, aliiomba wizara yenye dhamana na ardhi kuwasaidia kutatua mgogoro huo kwa kuwa hivi sasa wameshindwa kufanya shughuli yoyote na kila wanapoingia katika mashamba yao wanakamatwa na kuwekwa ndani.

Naye Rosemary Maganga, alisema wamekwenda kwa viongozi mbalimbali lakini hakuna suluhu waliyopatiwa zaidi ya kukamatwa na kuwekwa ndani kila wanapojaribu kufuatilia haki yao.

"Mwenyekiti wa kijiji hana msaada na sisi yeye ndiye amekua sababu ya sisi kukamatwa na kuwekwa ndani lakini hata kikao cha hivi karibu alikuja Mkuu wa Wilaya na tulipohoji kuhusu maeneo yetu na makaburi haya akatujibu kuwa katoeni mifupa yenu," alisema.

Aliongeza: "Kweli kiongozi tunayemtegemea anaweza kutujibu sisi katoeni mifupa yenu lakini ukisimama kuhoji kitu anasema weka matako yako chini na sisi watu wazima kweli Mkuu wa Wilaya anaweza kutujibu hivyo," alihoji.

Ofisa Utawala, Haki za Binadamu Afrika, Jafari Mnenwa, alisema mgogoro huo ni wa muda mrefu ambao wao pia wamejilidhisha kwa kufanya uchunguzi na kubaini kuwa serikali inapaswa kuchukua hatua ya kuumaliza.

Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Gift Msuya, akitolea ufafanuzi wa malalamiko hayo alisema mgogoro huo tayari walishaumaliza na eneo hilo limepimwa na kupatiwa hati miliki.

"Pale kweli kuna wazee walitoa eneo lao kwa ajili ya shule lakini hivi sasa wameibuka wajukuu wao ndiyo wanadai maeneo yale. Lakini tayari tulishapima ni eneo la hekari 57 na lina hati yake tayari," alisema Msuya.

Kuhusu kauli zisizo na staha kwa wananchi mkuu huyo wa wilaya alisema yeye kama mtumishi wa umma anayejitambua hawezi kumjibu mwananchi maneno kama hayo.



Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi Taifa (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba (kulia) na Katibu Mkuu wa CUF, Hamad Masudu Hamad (kushoto), wakimtambulisha aliyewahi kuwa Katibu wa CCM Wilaya ya Dodoma na Kiteto na Ofisa Mwandamizi Idara ya Mahusiano ya Kimataifa, Othman Dunga, baada ya kutangaza kujiunga na chama hicho kwenye mkutano uliofanyika stendi kuu ya mabasi ya zamani ya Kondoa jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## CUF yajipanga kushinda uchaguzi wa mitaa, mkuu

**Na Peter Mkwavila,** KONDOA

CHAMA cha Wananchi (CUF) kimesema kutokana na mikakati waliyojiwekea watahakikisha wanashinda katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Mwenyekiti wa chama hicho, Prof. Ibrahim Lipumba, alibainisha hayo juzi wilayani hapa alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa kuwatambulisha wanachama wapya zaidi ya 30 waliojiunga na chama hicho.

Mmoja waliojiunga ni aliyewahi kuwa Katibu wa CCM Wilaya ya Dodoma na Kiteto, Othman Dunga.

Prof. Lipumba alisema chama hicho kimejipanga kuhakikisha chaguzi zote za mwaka 2024 na 2025 wanashinda kwa kishindo kikubwa na kwa gharama yoyote.

Alisema ili kufanikisha azma hiyo wanachama wake wanapaswa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika daftari la wapigakura pamoja na kupiga kura na kuchagua viongozi wao ambao wana sifa.

Prof. Lipumba alisema kuwa ili chama kiweze kupata ushindi huo ni muhimu wanachama kujitokeza kwa wingi na kutekeleza jukumu hilo muhimu kwa vitendo.

Alisema CUF kimekusudia kushinda kwa kishindo kwa kuanzia nafasi zote ikiwamo wenyeviti, madiwani, ubunge hadi urais, lakini ni pale ambapo wanachama hao watakapojitokeza kuanzia hatua ya awali hadi ya mwisho.

Awali Katibu Mkuu wa CUF Taifa, Hamad Masoud Hamad, aliwataka wanachama kufanya siasa zenye ustaarabu na zenye hoja za msingi, ambazo zitakazoleta mabadiliko ya kiuchumi kwa njia ya amani.

Hamad alisema anaimani kuwa uchaguzi wa mwaka huu Watanzania hawatafanya makosa katika kuwachagua viongozi wabovu.

Naye Othman Dunga akizungumza kwenye mkutano huo baada ya kutambulishwa, alisema kuondokana kwake CCM anaenda kuleta mabadiliko kwa wananchi wa wilaya hiyo.

# Bil.17/- kujenga bwawa, miundombinu umwagiliaji

**Na Elisante John,** SINGIDA

SERIKALI imeingia mkataba wa ujenzi wa bwawa na mindombinu ya umwagiliaji, utakaogharimu zaidi ya Sh. bilioni 17. 705, na kuhudumia wananchi zaidi ya 16,000 wa Kata ya Msange Tarafa ya Ilongero Halmashauri ya Wilaya ya Singida.

Mradi huo ni sehemu ya miradi sita ya umwagiliaji, inayotekelezwa mkoani Singida, kati ya 100 nchini kote, ambayo Rais Samia Suluhu Hassan amedhamiria kuongeza uzalishaji na kukuza uchumi kwa wananchi, hasa kwa wananchi wanaoishi katika mikoa inayopata mvua mara moja kwa mwaka.

"Nimshukuru sana Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kutuletea mradi huu mkubwa, hii inadhihirisha wazi anatujali sisi watu wa Singida...nchi nzima kuna miradi 100, lakini ametupendelea sisi watu wa Singida, katupatia mabwawa sita ya umwagiliaji," alisema.

Katika hafla hiyo, kwa niaba ya serikali, kupitia Wizara ya Kilimo, chini ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Dendego alimtaka mkandarasi wa kampuni ya Kagwa Surprise Limited wa Singida, kutekeleza mradi huo kwa viwango, ili wananchi waweze kunufaika na matunda ya serikali.

Kuhusu changamoto zinazolalamikiwa na baadhi ya wananchi, yakiwamo madai ya fidia, Dendego aliahidi kukutana na walalamikaji na akisema anaamini atasimama imara kutatua kero hiyo.

Awali mhandisi wa umwagiliaji Mkoa wa Singida, kutoka Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Japheth Senyinah, alisema mkataba ni wa kipindi cha miaka miwili na utakamilika Julai 27 mwaka 2027, ukihusisha ujenzi wa bwawa, miundombinu ya umwagiliaji, nyumba za watumishi wa mradi na gari lenye thamani ya Sh. milioni 110, kwa ajili ya shughuli na majukumu mbalimbali ya mradi.

Diwani wa Kata ya Msange, ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Eliya Dighah, alisema kupitia makabidhiano hayo anaamini changamoto zinazotolewa na baadhi ya wasioutakia mazuri mradi, serikali itamaliza, tayari kwa ajili ya mradi kuanza uzalishaji.

Kupitia hadhara hiyo, Dighah aliishukuru serikali kufanikisha mradi huo wa bwawa, ambao una umuhimu mkubwa kwa ukombozi wa wakulima kutoka vijiji vinane, ambavyo ni Msange, Mangida, Sefunga, Ishipunga, Maghojoa, Mwasauya, Ghata na Mwachambia.

Mkandarasi wa ujenzi wa mradi huo, Evra Kagwa, aliahidi kutekeleza na kuukamilisha kwa wakati ili wakulima 3,000, waanze kunufaika kutokana na ekari 3,500 zilizopo eneo la mradi, lakini pia naamini watakaonufaika watakuwa zaidi ya hao, kutokana na uzalishaji wa mazao yatakayopatikana," alisema Kagwa.



# Mkandarasi ujenzi barabara nne atishia kugoma

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

UJENZI wa barabara ya njia nne katikati ya Jiji la Mbeya, umeanza kuingia dosari kutokana na mkandarasi anayetekeleza mradi huo kuanza kutishia kugoma kwa madai ya kutolipwa zaidi ya Sh. bilioni 12.9.

Aidha, mkandarasi huyo anashindwa kuendelea na mradi katika baadhi ya maeneo ya katikati mwa Jiji hilo kutokana na serikali kushindwa kuhamisha baadhi ya miundombinu muhimu ikiwamo ya maji ambayo inakwamisha kazi.

Barabara hiyo (Km 29) inayoanzia eneo la Nsalaga mpaka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe ni sehemu ya mradi wa Barabara ya Igawa-Tunduma (Km 218) pamoja na barabara ya mchepuko kwa ajili ya malori yenye urefu wa kilomita 48.9 ambao unatekelezwa kwa zaidi ya Sh. trilioni 1.3.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbeya Mjini, mwakilishi wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) Mkoa wa Mbeya, Frank Kamala alisema mkandarasi huyo amewasilisha barua ya kusudio la kusitisha kazi.

Alisema mkandarasi huyo tangu alipoanza kazi hajalipwa hata fedha za awali za ukusanyaji wa vifaa kwa ajili ya mradi huo na hivyo kushindwa kutekeleza mradi kwa ufanisi na kwamba amekuwa akiomba alipwe hata fedha kidogo ili aendelee na kazi.

"Tunaomba sana mtusaidie kutatua kero hizi, pale katikati ya mji ambapo pana makazi mengi ya watu pana mabomba makubwa yenye ukubwa wa nchi 16 ambayo hayajaondolewa na hivyo kusababisha mkandarasi ashindwe kuendelea na kazi," alisema Kamala.

Alisema ili mabomba hayo yaondolewe zinahitajika zaidi ya Sh. bilioni mbili ambazo kampuni inayosambaza mabomba imeyaainisha lakini serikali haijatoa fedha hizo na hivyo kusababisha mradi kuendelea kuchelewa.

Alisema mabomba hayo yasipoondolewa mradi hauwezi kuendelea kutekelezwa kwa maelezo kuwa unaweza kusababisha wananchi wakakosa huduma ya maji.

Hata hivyo alisema tatizo lingine lililosababisha ujenzi wa barabara hiyo kuchelewa kuanza ni uthamini kuchelewa kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo migogoro ya ardhi na migogoro ya miradhi baina ya ndugu.

Alisema uthamini wa awali ulifanyika mwaka 2020 lakini wananchi hawakulipwa na hivyo serikali ikalazimika kufanya uthamini mwingine mwaka 2023 ambao pia ulikwamishwa na migogoro ya ardhi na mirathi na uthamini wa mwisho umefanyika mwaka huu.

Alisema uthamini umekamilika na wananchi wameridhia kulipwa fidia na kwamba kwa sasa kinachosubiriwa ni majedwali kupelekwa kwa Mkuu wa Wilaya ili asaini na kisha kupelekwa kwa Mthamini Mkuu wa Serikali ili aidhinishe na wananchi walipwe.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbeya Mjini, Afrey Nsomba, alisema mradi huo ni miongoni mwa miradi muhimu ambayo inatakiwa kukamilika kwa wakati ili wananchi waendelee kupata huduma wanazostahili.

Alisema watalifikisha jambo hilo kwenye mamlaka zinazotakiwa ili lishughulikiwe na kumalizika, huku akidai kuwa walishawaaminisha wananchi kuwa mradi huo utakamilika ndani ya miaka miwili.

"Hili ni la kwetu tunalichukua kwamba mradi unasuasua kwa sababu mkandarasi anachelewa kupata fedha, tunatakiwa tuwe na majibu sahihi ili hata wananchi wakihoji tuweze kuwaeleza kwa sababu tunaelekea kwenye uchaguzi," alisema Nsomba.

Akiwa ziarani jijini Mbeya, Naibu Katibu Mkuu wa CCM Bara, John Mongela, aliwasilishiwa kero ya barabara hiyo na viongozi wa chama hicho mkoa na akaahidi kufuatilia ili fedha zipatikane na mradi uendelee.

Alisema atawasiliana na Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba na viongozi wengine wa juu wa serikali ili wajadiliane namna ya kupata fedha hizo na mkandarasi aendelee na kazi.



Baadhi ya vijana wakiendelea na shughuli yao ya kusafirisha mizigo kwa kutumia matoroli kwenda kwenye maeneo ya kuhifadhia katika Soko la Sido jijini Mbeya baada ya kuishusha kwenye malori mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wanaoweka taarifa binafsi mitandao jamii waonywa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wametakiwa kutumia vizuri mitandao ya kijamii ikiwa ni pamoja na kuepuka kuweka taarifa zao za siri ili zisidukuliwe na watu wenye nia ovu na wakazitumia kwenye matukio ya uhalifu.

Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Tekonojia ya Habari, Maryprisca Mahundi, alitoa wito huo mwishoni mwa wiki alipozungumza na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mbeya (CUoM) pamoja na wahadhiri.

Alisema baadhi ya watu wamekuwa wakidukua taarifa muhimu za watu wengine kwenye mitandao na kuzitumia kukopa fedha kwenye taasisi zinazokopesha kupitia mitandao na kuwaweka wahusika kama wadhamini.

Alisema wanaposhindwa kurejesha mikopo hiyo ndipo taasisi hizo zinaibuka na kuanza kutuma jumbe zenye vitisho na hapo ndipo wahusika wanaanza kushtuka na kulalamika bila kujua kwamba walisababisha wao wenyewe kwa kuweka taarifa zao muhimu mitandaoni.

"Hivi karibuni Rais Samia alituzindulia taasisi ya kulinda taarifa binafsi, lakini bado kuna watu ni watundu huko kwenye mitandao, wanaweza kuchukua taarifa zako na kuzitumia vibaya, jitahidi usiweke taarifa zako muhimu huko," alisema Mahundi.

Makamu Mkuu wa CUoM, Prof. Romuald Haule alisema waliandaa kongamano maalumu la kuadhimisha mwaka mmoja wa chuo hicho tangu kilipopanda hadhi.

Alisema lengo la kongamano hilo ni watumishi pamoja na wanafunzi kutafakari maendeleo yao waliyoyapata katika kipindi cha mwaka mmoja na malengo ya mwaka unaofuata.

# Wawili wafariki dunia ajali ya lori, IT

**Na Elizabeth John,**
WANGING'OMBE

WATU wawili wamefariki dunia baada ya gari walilokuwa wakisafiria lenye namba 5103 IT ikitoka Dar es Salaam kwenda Tunduma kugongana na lori la mizigo lenye namba za usajili T540 DZW.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi, Mahamoud Banga, alisema tukio hilo lilitokea Julai 13 saa 12 asubuhi katika Kijiji cha Litundu wilayani Wanging'ombe katika Barabara Kuu ya Makambako-Mbeya.

Kamanda huyo aliwataja waliofariki katika ajali hiyo kuwa ni Baharuni Hatimu Nyalusi (31) ambaye ni dereva wa IT na Emmanuel Ambakisye ambaye ni abiria na wote walikuwa wamepanda kwenye gari ndogo.

"Gari hilo la mizigo lilikuwa limebeba mchele likitoka mkoani Mbeya kwenda mkoani Arusha na chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi ambapo dereva wa gari ndogo alikuwa anajaribu kuyapita magari mengine bila kuchukuwa tahadhari," alisema Kamanda Banga. Alisema miili ya waliofariki imefikishwa Kituo cha Afya Wangig'ombe kwa ajili ya uchunguzi zaidi na hivyo kutoa rai kwa madereva wa masafa marefu kuwa makini na kuzingatia sheria za usalama barabarani.

Alisema kutokana na mwendokasi aliokuwa nao dereva wa gari ndogo, dereva wa lori alishindwa kumkwepa na hivyo wakagongana.

Dereva wa lori hilo, Makeke John alisema kwenye gari hilo alikuwa peke yake na alikuwa anatokea Ubaruku wilayani Mbarali kuelekea Arusha ambako alikuwa anapeleka mchele.

Alisema yeye hakupata madhara kwenye ajali hiyo isipokuwa uharibifu ulitokea kwenye gari yake ambalo liliharibika mbele, huku akieleza kuwa alikuwa hana namna yoyote ya kunusuru kusitokee ajali hiyo kutokana na mwendo waliokuwa nao.

"Dereva wa hii gari ndogo akawa anayapita magari mawili yaliyokuwa mbele yake, mimi ningetaka kumwokoa ningesababisha maafa zaidi kwa watu waliokuwa kwenye magari yale mawili maana ilitakiwa nihamie upande wao na ningewagonga maana ilikuwa ghafla," alisema John.

Mmoja wa mashuhuda wa ajali hiyo, Winfred Mchakafu alisema akiwa anatokea nyumbani kwake kuelekea kwenye majukumu yake aliona magari matatu yakiwa yameongozana lakini gari ndogo iliyokuwa nyuma ikawa inayapita mengine. Alisema muda mfupi baadaye alisikia kishindo kikubwa na alipokwenda kushuhudia alikuta vumbi limetimka na magari hayaonekani ndipo akabaini kwamba ilikuwa ni ajali.

Alisema baadaye walishirikiana na watu wengine kuwaokoa watu waliokuwa kwenye gari ndogo lakini walikuwa wameshafariki.

## UN yataja siri mafanikio Dira ya Maendeleo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (UNICEF) Ofisi ya Zanzibar, Laxmi Majj Bhawani, amesema ili kufikia Dira ya Maendeleo ya Mwaka 5050 lazima watoto wapate huduma bora ya afya lishe, mzingira salama, elimu bora na kulindwa na ukatili wa kila aina.

Aliyasema hayo alipokuwa akizungumza katika mafunzo kwa waandishi wa habari yaliyofanyika katika ofisi za UNDP zilizopo Kinazini Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Laxmi alisema yakitekelezwa hayo watoto wanaweza kujifunza kukua vizuri na kuwa na uwezo wa kufanya kazi na kuchangia maendeleo ya kifamilia na kiuchumi.

Alisema UNICEF inafanya kazi kwa karibu na serikali pamoja na asasi za kiraia na wadau mbalimbali katika kuhakikisha mtoto atapatiwa huduma hizo.

Alisema kuwa watoto wanapaswa kupatiwa mambo ya msingi katika makuzi ili kujenga mwelekeo mzuri wa mustakabali wa maisha yao ya baadaye.

Mshauri wa Ushirikiano wa UNICEF, Dk. Ladislaus Batinoliho, alisema kuwa lengo la mafunzo hayo ni kuendelea kuhamasishana na kuwa na hari mpya na moyo zaidi wa kuendelea kumlinda mtoto.

Aidha, alisema kuwa vyombo vya habari ni muhimili katika serikali na ndiyo maana UNICEF kwa kuliona hilo wameona ni vyema wakatoa mafunzo hayo.

"Pia tunatamani baada ya siku ya leo katika habari unayoiandika angalau japo habari moja imguse mtoto, tulinde watoto wetu kwa sababu tunafanya hivi kwa kujua kwamba nyinyi ni muhimili wa nne mkubwa na hatuwezi kulinda haki za mtoto kama hatujawahusisha nyinyi," alisema.

Mtaalamu wa Ulinzi wa Watoto kutoka UNICEF, Ahmed Rashid Ali, alisema Zanzibar imepiga hatua kubwa katika ulinzi wa mtoto na ili hatua hizo ziweze kuongezeka zaidi wanahitaji kulindwa.

Ofisa kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, Wanawake na Watoto, Nyezuma Simai Issa, alisema ulinzi wa mtoto ni jukumu la kila mtu ili aweze kukua katika misingi imara inayotakiwa na kuwa raia mwema mwenye kutegemewa na familia yake na taifa kwa ujumla.

Hata hivyo alisema kuwa katika Mkataba wa Kimataifa wa Kumlinda Mtoto Kipengele cha 19 kimesisitiza kila nchi ambayo imeridhia mkataba huo kuweka mifumo madhubuti ya ulinzi wa mtoto katika nchi yake.

# Wajasiriamali watakiwa kuchangamkia mikopo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAJASIRIAMALI wanawake wametakiwa kuchangamkia fursa za kilimo cha mazao ya baharini kwa kuomba mikopo nafuu ambayo milango yake imefunguliwa na Benki ya Jumuiya ya Ulaya (EIB) pamoja na Umoja wa Ulaya (EU).

Wito huo umetolewa na Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mgeni Hassan Juma, katika ziara ya kuwatembelea wakulima wa mwani.

Alisema uchumi wa bluu kupitia kilimo cha mazao ya baharini ndio vipaumbele vya Serikali ya Zanzibar ambapo wanawake ni walengwa wakubwa.

Alisema katika Bajeti ya Serikali ya Zanzibar Sh. bilioni 230 zimetengwa kwa ajili ya kuwawezesha wakulima wa mwani na wafugaji wa mazao ya baharini kujiendeleza na kujikwamua na umaskini.

Aidha alisema juhudi za Serikali ya Zanzibar kuwashirikisha wadau wa maendeleo zimefanikiwa ambapo EIB pamoja EU zimetoa Sh. trilioni 1.043 ambazo zitakwenda kwa taasisi za fedha kuwakopesha wajasiriamali wa kilimo cha mazao ya baharini.

"Wakulima wa mazao ya baharini ikiwamo mwani mnatakiwa kuchangamkia fursa za fedha za mikopo nafuu kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha mazao ya baharini pamoja na ufugaji wa matango baharini na samaki," alisema.

Mkurugenzi wa Idara ya Ustawi wa Jamii, Siti Abasi, aliwataka wanawake kuchangamkia fursa hizo ambazo ndiyo zitakazowainua kiuchumi na kupiga hatua kubwa ya maendeleo.

Alisema uchumi wa bluu zipo fursa nyingi ambazo zinatakiwa kuchangamkiwa na wakulima wa mazao ya baharini.

Baadhi ya wakulima wa kilimo cha mwani waliotembelewa waliahidi kufuata utaratibu ambao utawawezesha kupata fedha hizo ili kuendesha shughuli zao, ikiwamo kuimarisha mashamba ya mwani yaliopo baharini.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Bluu, Zahoro Al-kharousy, alivitaka vikundi vya wajasiriamali kuchangamkia fursa hizo na kuwasilisha maombi ya fedha za mikopo nafuu haraka.



Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Jenifa Christian Omolo, akikabidhi zawadi kwa Mkuu wa Kituo cha Huduma cha SAFAAD, Adolph Alfred, kwa niaba ya Kikundi cha Umoja wa Wanawake wa Wizara ya Fedha (Golden Women) walipotembelea kituo hicho na kutoa mahitaji mbalimbali kuelekea kilele cha Siku ya Wanawake. **PICHA: WIZARA YA FEDHA**

# Watoto wenye mahitaji maalum kujifunza masomo kwa michezo

**Na Gwamaka Alipipi**

WATOTO wakiwamo wenye mahitaji maalum kutoka mkoani Arusha na Mara wanatarajia kushiriki katika shughuli za kujiendeleza kielimu, hususani zinazolenga kuhamasisha kujifunza kupitia michezo.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ziara hiyo iliyopewa jina la 'Ziara ya kujenga akili', Mkurugenzi wa Mawasiliano na Maendeleo wa Shirika la Ubongo, Iman Lipumba alisema itaanza leo na watashirikiana na Taasisi ya Vodacom Tanzania pamoja na Shirika la Kimataifa la Hope and Healing.

Alisema ziara hiyo inalenga kutoa uzoefu wa kielimu unaovutia na wenye matokeo kwa watoto na walezi kote nchini, hususani kwa wenye mahitaji maalum.

"Ubongo, tumejitolea kutoa maudhui ya kielimu ambayo yanawawezesha kizazi kijacho cha viongozi wa Afrika. Ni kielelezo cha dhamira yetu ya kufikia watoto kila kona ya Tanzania, kuhakikisha wanapata rasilimali na fursa za kustawi." Alisema Iman.

Iman alisema watawashirikisha watoto kwa michezo ya kielimu na mashindano, ikijumuisha matamasha ya mwisho wa wiki katika kila mkoa ambapo watoto na walezi wao watashiriki katika shughuli mbalimbali.

"Wakati wa sherehe hizi, watoto na walezi watapokea bidhaa za kipekee na nyenzo za kufundishia ili kusaidia safari yao ya masomo," alisema.

Alisema ziara hiyo pia itahusisha maonesho na uwezeshaji wa programu ya Ubongo PlayRoom na jukwaa la e-Fahamu la Vodacom Tanzania Foundation. Iman alisema programu ya Ubongo PlayRoom hutoa mazingira mazuri na yasiyokatizwa ya kujifunzia, ikijumuisha video, sauti, vitabu na michezo iliyoratibiwa.

Alisema vitu vyote hivyo vimewekwa sehemu moja, kwamba programu inakusanya maudhui yote asili ya Ubongo katika nafasi moja, kuhakikisha usambazaji kwa urahisi na ugunduzi wa maudhui.

Iman alisema e-Fahamu huwapa walimu nyenzo za kuboresha uwasilishaji wao wa masomo, pia inawapa wanafunzi uwezo wa kufikia maudhui ya kina ya kujifunza, kuwawezesha kujisomea na kuelewa kwa kina wanapofundishwa darasani.

"Tunafuraha kuunga mkono ziara hii ya kujenga akili ya Ubongo ya mwaka 2024 kama sehemu ya dhamira yetu ya kuboresha masomo ya watoto nchini Tanzania. Tunaamini kwa pamoja tutafanikisha elimu inakuwa bora nchini na inapatikana kwa kila mtoto," alisema Sandra Oswald, Meneja wa Vodacom Tanzania Foundation."

Alisema kupitia ushirikiano huo jukwaa la ubunifu la e-Fahamu la Vodacom Foundation litaunganishwa na maudhui ya elimu ya kuvutia ya Ubongo na kutoa mchanganyiko wenye nguvu wa teknolojia na ubunifu.

Mtaalamu wa Maendeleo ya Mtoto kutoka Shirika la Hope and Healing International, Kendra-Lee Heney alisema: "Tumejitolea kuhakikisha watoto wenye ulemavu nchini Tanzania wanaweza kushiriki kwa uhuru katika burudani ya Ubongo, elimu na programu za kujenga kujiamini".

# Watakiwa kujiunga kikoa Dot Tz kuongeza mapato

**Na Mauld Mmbaga**

WATANZANIA wametakiwa kujisajili kutumia kikoa cha Taifa cha Dot Tz kuchangia ongezeko la mapato ya taifa na ukuaji wa uchumi nchini.

Kauli hiyo ilitolewa Dar es Salaam jana na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk. Jabiri Bakari, alipozungumza katika Maonesho ya 48 ya Kibiashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF).

Alisema kikoa cha Dot Tz ni utambulisho wa Tanzania katika anga la mtandao kipo kama namba ya simu ya +255 ambayo inaitambulisha nchi kama simu inayotumika nchini.

"Mtandaoni kuna utambulisho wa aina nyingi wa mataifa tofauti hivyo faida za matumizi yake ni kusimamiwa nchini hivyo mtu atachangia katika ukuaji wa pato la taifa na uchumi kwa sababu mtu anapofanya malipo anafanya katika taasisi ambazo zimesajiliwa Tanzania hivyo na wewe unakuwa sehemu ya uchangiaji na ukuaji wa uchumi," alisema.

Dk. Bakari alitaja faida nyingine ni mtu akipata matatizo anaweza kutafutiwa suluhisho na taasisi zilizoelekezwa Tanzania wakiwamo TCRA hivyo mtu akitumia kikoa kingine cha dot.com au dot org kwa sababu kinasimamia nchi nyingine utakapopata changamoto za kiufundi Tanzania haitaweza kukutafutia suluhisho.

"Kwa upande wa malipo, unapochelewe kufanya malipo ya vikoa vingine kama dot com, dot org kunakuwa na penati ya zaidi ya dola za kimarekani 100 na kupelekea kufungwa kwa kikoa chako, lakini kwa Tanzania hakuna penati ya kikoa na mtu hayupo kwenye risk (hatari) ya kufungiwa kikoa chake," alisema.



Aidha, alitaja faida nyingine ni kuwa utambulisho wa biashara kama Mtanzania kwa sababu duniani wafanyabiashara ni wengi unavyotumia kikoa cha dot tz mtu hufahamu biashara fulani humilikiwa na Mtanzania.

Kikoa hicho kinatoa ushindani sawa kibiashara mtandaoni kwa maana ya kuwezesha biashara ya mtu kuwa kipaumbele cha upatikanaji wa taarifa zilizopo nchini mtandaoni.

"Mwamko wa mashirika kujisajili ni mzuri kwa sababu tuna wasajili zaidi ya 70 na watu waliosajiliwa ni zaidi ya 30,000 na tunahitaji hii idadi izidi kuongezeka mwisho wa siku watu waachane kutumia dot com, dot org na vikoa vya mataifa mengine na kujifunza kutumia vya kwetu," alisema.

Hata hivyo, alisema kikoa hicho cha dot tz ni rasilimali ya nchi ambayo ni kwa ajili ya mawasiliano kwenye intaneti kupitia tovuti au barua pepe ambayo kila nchi inakuwa na utambulisho wa kipekee na kwa Tanzania ni kikoa hicho.

## KUPOTEA KWA CHETI



**SHABANI HALIBU RAJABU,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha Kidato cha nne chenye index namba **CS 17000282188** kilichotolewa na Baraza la mitihani kupitia shule ya Sekondari ya Himo Secondary School. Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa polisi: **PHQ/ KIL/MOS/15836/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na.26/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU RASHID JOHN MWIGUNE wa MAILI MBILI DODOMA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SCOLASTICA JOHN GEDA**

**TANGAZO**
**(Kanuniya 5(2) ya Kanuniza Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 31 Mwezi 07 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo Tarehe 08 Mwezi 07 Mwaka 2024.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PETER ASAN MALUGU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T547BTR** aina ya **Suzuki CARRY,** Chassis No. **DC51T226605,** Engine No. **F6AJAAI010542.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/TEM/141550/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HOPE SILVESTER NZALI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 122 EDW** aina ya **RANGE.** Chassis namba **SALLSAAF3AA243092.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **WMB/RB/1938/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CLARA DISMAS MWAKITOSI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 676 ACZ** aina ya **TOYOTA DYNA.** Chassis namba **BU600026608.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/141581/2024**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No 16454 Of 2024**

**In the matter of the estate of the late DANIEL ANAEL LEMA of Kikuyu Kaskazini within Dodoma City.**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by ENNE ANAEL LEMA.**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 14 THday of August...................... 2024

Dated at Dodoma this 11TH day of JULY................2024

RESIDENT MAGISTRATE



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisikiliza wimbo wa kuabudu wakati alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika Maadhimisho ya Miaka 85 ya Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG) Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# PURA yaita wawekezaji utafutaji, uchakataji gesi

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), imewaalika wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi kuwekeza katika miradi ya utafutaji na uchakataji wa gesi asilia nchini.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya PURA, Khalfan Khalfan, alipotembelea banda ya mamlaka hiyo kwenye Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) yanayoendelea kwenye Viwanja vya Mwalimu Nyerere Barabara ya Kilwa, Temeke.

Alisema wawekezaji wanaruhusiwa kuwekeza hata kwenye utafutaji na kwamba sio lazima kusubiri wanaotoka nje ya nchi pekee.

"Kinachohitajika hapo kikubwa ni utaalamu na uwezo na kipaumbele cha serikali kwa sasa ni kuhakikisha kwamba tunaongeza wawekezaji kwenye utafutaji, kwa sababu kwa kipindi kirefu tumekuwa hatuna wawekezaji wa kutosha na maeneo mengine yalikuwa na wawekezaji, lakini kisheria wamerudisha serikalini."

"Kwa hiyo sisi kama PURA tuna jukumu la kutafuta wawekezaji kwenye hayo maeneo ambayo yako wazi," alisema Khalfan.

Kadhalika, alisema wanatarajia kuendesha mkutano wa kutangaza maeneo ya uwekezaji pamoja na kushindanisha wawekezaji hao.

"Tumekuwa tukifanya matayarisho ya duru, sheria ya mafuta inasema kwamba wawekezaji watafutwe kwa ushindani sio kwa kuokotwa na ili wapatikane kwa ushindani inafanyika duru ambayo ni mkutano wa kutangaza maeneo, wawekezaji wanakuja wanasikiliza halafu wanachagua yale wanayotaka ndio wanaleta maombi ya kuja kuwekeza kwenye hayo maeneo."

"Tumekuwa tukifanya hayo matayarisho kwa muda sasa, siyo kazi ndogo, lakini hatimaye tunaona mwanga, huenda ile duru ikafanyika robo ya kwanza ya mwaka ujao," alisema Khalfan.

Pia alisema wamekuwa wakifanya mazungumzo ya kutafuta wawekezaji katika mradi wa kuchataka gesi asilia wa Likongo, mkoani Lindi na mazungumzo hayo yanaendelea vizuri.

Alisema asilimia kubwa ya gesi asilia itakayopatikana katika mradi huo itakuwa inauzwa nje ya nchi.

"Na huo pia utakuwa ni jukumu la PURA kusimamia shughuli zote za uchakataji, uuzaji na kuangalia kama serikali inapata mapato yake halali kwenye shughuli hiyo," alisema.

# Polisi wachunguzwa kuhusu miili iliyotupwa Kenya

**NAIROBI,** Kenya

MAMLAKA huru inayosimamia jeshi la polisi nchini Kenya (IPOA) imesema inachunguza polisi waliohusika kwa njia yoyote kufuatia ugunduzi wa miili iliyokatwakatwa na kutupwa kwenye shimo la jalala mjini Nairobi.

Awali polisi walisema miili kadhaa iliyokatwakatwa ya wanawake sita iliyofungwa kwenye mifuko ya plastiki ilipatikana siku ya Ijumaa ikiwa imetupwa kwenye jalala la taka katika timbo isiyotumika huko Mukuru, kusini mwa mji mkuu wa Nairobi.

Mamlaka ya IPOA ilisema katika taarifa baadaye kwamba mabaki ya watu takribani tisa ilikuwa imegunduliwa, saba ya wanawake, na kuitisha uchunguzi wa haraka ufanyike kuitambua.

"Miili iliyofungwa kwenye mifuko na kamba za nailoni, ilikuwa na alama za wazi za mateso ya kukatwakatwa," ilisema mamlaka hiyo, ikidokeza kwamba jalala hilo lilikuwa chini ya mita 100 kutoka kituo cha polisi.

Aidha, ilielezwa kuwa polisi wa Kenya wanakabiliwa na ukosoaji na shinikizo baada ya watu kadhaa kuuliwa wakati wa maandamano ya mwezi uliopita, huku mashirika ya kutetea haki za binadamu yakiwatuhumu maofisa hao kwa kutumia nguvu kupita kiasi.

> **Huku uchunguzi wa polisi ukiendelea, IPOA kwa uangalifu inafanya uchunguzi wa awali kubaini kama kulikuwa na uhusikaji wowote wa polisi katika vifo hivyo, au kushindwa kuchukua hatua kuvizuia**

Umati wa watu waliokusanyika Ijumaa katika eneo kulikopatikana miili walikuwa wakipiga kelele wakisema "Ruto lazima aende", iliyokuwa kauli mbiu ya wimbi la maandamano yaliyoongozwa na vijana Wakenya maarufu Gen Z.

Ilielezwa kuwa polisi ya Kenya wanaogopwa na hukabiliwa na madai ya mara kwa mara ya mauaji kinyume cha sheria lakini ni nadra kushtakiwa na kuhukumiwa.

Picha kwenye televisheni nchini humo ziliwaonyesha watu wakitumia kamba kuopoa magunia yaliyokuwa na mabaki ya miili ya binadamu kutoka kwenye maji yaliyojaa taka katika jalala la kwenye timbo huko Mukuru.

"Huku uchunguzi wa polisi ukiendelea, IPOA kwa uangalifu inafanya uchunguzi wa awali kubaini kama kulikuwa na uhusikaji wowote wa polisi katika vifo hivyo, au kushindwa kuchukua hatua kuvizuia," mamlaka hiyo ilisema.

Kurugenzi ya uchunguzi wa makosa ya jinai ilisema uchunguzi unapendekeza wahanga wote waliuawa kwa aina moja, bila kutoa maelezo zaidi.

Ofisi ya mwendesha mashtaka ya umma pia iliangazia eneo ilipopatikana miili hiyo kuwa karibu sana na kituo cha polisi na kusema ina wasiwasi mkubwa kuhusu ugunduzi huo unaoashiria ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu.

Ilielekeza polisi kuwasilisha matokeo ya uchunguzi wao katika kipindi cha siku 21, na pia kuzihimiza wakala za dola ikiwemo mamlaka huru ya IPOA kufanya uchunguzi kuhusu ripoti za watu kupotezwa kwa kutumia nguvu na vifo vinavyodaiwa kufanywa na polisi.

Tume ya haki za binadamu ya Kenya, asasi isiyo ya kiserikali, ilisema ilikuwa pia inahimiza uchunguzi wa kina ufanyike kubaini chanzo cha vifo hivyo na kuwatambua waliohusika. **AFP**



Aliyekuwa Rais wa zamani wa Marekani, Donald Trump, akilindwa na maofisa wa Idara ya ujasusi wa taifa hilo baada ya shambulio la risasi dhidi yake juzi. **PICHA: REUTER**

# Donald Trump: Naendelea salama nawashukuru FBI

**WASHINGTON,** Marekani

ALIYEKUWA rais wa zamani wa Marekani Donald Trump amesema anaendelea vizuri baada ya kufanyiwa shambulio la risasi, huku akiwashukuru maofisa wa usalama (FBI) kwa kutekeleza wajibu wao na kutoa majibu ya haraka juu ya tukio hilo.

Hiyo ni kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana kwenye tovuti ya nje ya Kamati ya Kitaifa ya Republican (RNC), tukio la kushambuliwa kwa Trump lilitokea juzi wakati akihutubia kwenye mkutano wa hadhara katika jimbo la Pennsylvania.

Ilielezwa kuwa wakati akiendelea na mkutano huo mtu mmoja alifyatua risasi kadhaa na kumjeruhi Trump sikioni.

Shirika la upelelezi la Marekani la FBI lilisema mwanamume huyo aliyeuawa mara tu baada ya kufanya shambulio hilo, ametambuliwa kuwa ni Thomas Crooks (20) na mkazi wa jimbo la Pennsylvania. Na kwamba uchunguzi zaidi kuhusu tukio hilo unaendelea.

Taarifa ya kampeni ya Trump na RNC ilisema "Nanatarajia kuungana nanyi nyote huko Milwaukee tunapoendelea na kongamano letu la kumteua kuhudumu kama rais wa 47 wa Marekani. Akiwa mteule wa chama chetu... ataendelea kushiriki maono yake ya 'Make America Great Again'."

> **Kikubwa zaidi naomba nitoe salamu za rambirambi kwa familia ya mtu aliyekuwa kwenye mkutano wa hadhara aliyeuawa, na pia kwa familia ya mtu mwingine aliyejeruhiwa vibaya, ni jambo la ajabu kuwa kitendo cha aina hii kinaweza kutokea katika nchi yetu.**

"Kikubwa zaidi naomba nitoe salamu za rambirambi kwa familia ya mtu aliyekuwa kwenye mkutano wa hadhara aliyeuawa, na pia kwa familia ya mtu mwingine aliyejeruhiwa vibaya, ni jambo la ajabu kuwa kitendo cha aina hii kinaweza kutokea katika nchi yetu, " alisema.

"Hakuna kinachojulikana kwa wakati huu kuhusu mpiga risasi ambaye sasa amekufa. Nilipigwa risasi na kupenya sehemu ya juu ya sikio langu la kulia. Nilijua mara moja kuwa kuna kitu kibaya kwa kuwa nilisikia sauti ya kishindo, milio na risasi.

"Mara nikahisi risasi ikipasua kwenye ngozi. Kutokwa na damu nyingi kulitokea, kwa hivyo nikagundua ni nini kilikuwa kinatokea. Mungu Ibariki Marekani!" alisema kupitia taarifa hiyo.

Shirika la Ujasusi la Marekani lilisema linachunguza jaribio hilo, huku watu walioshuhudia tukio husika wakisema walimuona mtu mwenye silaha kabla ya shambulio hilo na waliziarifu mamlaka.

Hata hivyo, polisi walisema walipokea taarifa kadhaa za shughuli zenye kutia shaka, bila kufafanua zaidi.

Rais wa Taifa hilo, Joe Biden, alilaani shambulio hilo dhidi ya Trump na kusema kuwa matukio ya aina hiyo hayana nafasi katika taifa hilo.

Viongozi wa mataifa mbalimbali duniani pia walilaani shambulio hilo, huku Msemaji wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, akiliita tukio hilo kuwa ni vurugu za kisiasa.

Kansela wa Ujerumani, Olaf Scholz alitaja kitendo hicho kuwa cha chuki, wakati Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron akimtakia Trump nafuu ya haraka.

Naye Waziri Mkuu wa Uingereza, Keir Starmer, alisema amefedheheshwa na kushtushwa na kilichotokea na ametuma salamu za pole kwa walioathiriwa katika tukio hilo.

Miongoni mwa viongozi wengine waliolaani tukio hilo na kutoa pole kwa Trump ni pamoja na Rais wa Halmashauri Kuu ya Umoja wa Ulaya (EU), Ursula von der Leyen, na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya kujihami ya (NATO), Jens Stoltenberg.

Wengine ni Waziri Mkuu wa Canada, Justin Trudeau, Fumio Kishida wa Japan, Narendra Modi wa India na Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky. **BBC, DW**

# MGUNDA, UFUDU RASMI WAIBUKIA MASHUJAA FC

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mashujaa imetangaza kuwasajili straika Ismail Mgunda kutoka Singida Black Stars na kiungo mshambuliaji kutoka Kagera Sugar, Ally Nassor 'Ufudu' kwa ajili ya kuboresha kikosi chao kuelekea Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Taarifa iliyotolewa jana na Idara ya Habari na Mawasiliano ya klabu hiyo imesema mbali na wachezaji hao, pia imesajili wachezaji wawili kutoka KenGold, beki wa kulia kutoka KenGold, Robert Mathias na kiungo mshambuliaji, Yusuph Dunia.

"Tumesajili wachezaji watatu wapya, Mgunda kutoka Singida, ambaye ni mshambuliaji, atakitumikia kikosi chetu msimu ujao wa mashindano, tumempata 'mbavu ya kulia', Robert 'Makidala' akitokea KenGold na kiungo wa 'boli', Ufudu, na wenzake Dunia kutoka KenGold," ilisema taarifa ya Mashujaa FC.

Mashujaa FC yenye maskani yake Kigoma, ambayo ilianza kucheza Ligi Kuu msimu uliopita imeanza kwa usajili huo, baada ya kuondokewa na wachezaji watatu ambao ni Adam Adam aliyetimkia Azam FC, Omari Omari, aliyejiunga na Simba na Reliants Lusajo, ambaye taarifa zinasema huenda akatangazwa kwenye kikosi cha Dodoma Jiji FC hivi karibuni.

Aidha, kikosi hicho kinatarajia kuondoka Kigoma kwenda kupiga kambi mjini Zanzibar kwa ajili ya matayarisho ya mashindano msimu ujao ambayo ni Ligi Kuu Tanzania na Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), maarufu Kombe la FA.

**FUKUZIA...**



Winga wa Canada, Jacob Shaffelburg, akiambaa na mpira huku kiungo wa Uruguay, Nahitan Michel Nandez, akihaha kumfukuzia ili kumzuia kwenye mechi ya kusaka mshindi wa tatu wa michuano ya Copa Amerika 2024, iliyopigwa Marekani juzi na kumalizika kwa sare ya mabao 2-2 na kisha Uruguay kushinda kwa mikwaju ya penalti 4-3. **PICHA: MTANDAO**

# *Mafunzo kusajili wachezaji wapya sita*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

UONGOZI wa Klabu ya Mafunzo, umesema umejipanga kufanyia maboresho makubwa timu yake ili kuwa na mwanzo mzuri kwenye Ligi Kuu kuelekea msimu mpya wa 2024/2025.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa timu hiyo inayocheza Ligi Kuu Zanzibar, Hafidh Dege, alisema miongoni mwa maboresho hayo ni kufanya usajili ambao utaiwezesha timu hiyo kufanya vizuri ikilinganishwa na misimu miwili iliyopita.

Alisema hadi kufikia sasa timu hiyo imepanga kusajili wachezaji sita huku wakiwatema nane.

Dege alisema usajili huo utakwenda sambamba na mapendekezo ya benchi la ufundi la timu hiyo kwa kuangalia mapungufu ya msimu uliopita.

Alifafanua kuwa wachezaji hao sita watakaowasajili wapo ambao watatoka Tanzania Bara, na kwamba bado hawana uwezo wa kusajili mchezaji kutoka nje ya Tanzania.

"Msimu uliopita mzunguko wa kwanza hatukufanya vizuri, ingawa mzunguko wa pili tuliimarika, hivyo msimu huu hatutaki kubahatisha tunataka kuwa bora kuanzia mwanzo wa msimu," alisema.

Aidha, alisema katika kusajili wachezaji hao hawataki kufanya makosa, hivyo watakuwa makini katika kufuatilia taarifa zao kwa timu walizotoka.

Hata hivyo, alisema ni mapema kutaja majina ama klabu waliochezea wachezaji hao ambao wanawasajili.

# Kagera Sugar yaanza kujifua Ziwa Victoria

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha wachezaji wa Kagera Sugar, kimeanza maandalizi ya msimu mpya wa mashindano katika Fukwe za Ziwa Victoria, kikiwa na wachezaji wapya na wale wa msimu uliopita ambao wamesalia.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Hamisi Mazanzala, amesema wachezaji karibu wote wameshawasili na wameanza mazoezi ya kujenga miili yao nyakati za asubuhi na jioni wanayafanya kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba.

"Kila kitu kinakwenda kama kilivyopangwa, tumeshaanza mazoezi rasmi na tunatarajia msimu ujao tutafanya mambo makubwa zaidi," alisema.

Klabu hiyo imechapisha picha za video fupi kwenye mtandao wao wa kijamii wa instagram, ukionyesha wachezaji wa kikosi hicho wakifanya mazoezi kwenye fukwe za Ziwa Victoria, ambapo walionekana wakikimbia kwenye mchanga, huku wakiruka viunzi ambavyo vimewekwa maalum kwa ajili ya kazi hiyo.

Pia zipo video fupi zinazowaonyesha wakiwa wanakimbia kwa kuzunguka uwanja wa Kaitaba, yakiwa ni mazoezi ya kusaka pumzi na utimamu wa mwili kwa wachezaji, kabla ya kuanza ufundi.

Kikosi hicho kwa sasa kinanolewa na Fred Felix Minziro (pichani), ambaye alichukua nafasi ya Macky Mexime katikati ya Ligi Kuu msimu uliopita, aliyekwenda Ihefu, baadaye ikawa Singida Black Stars, lakini sasa anaifundisha Dodoma Jiji.

Msimu uliopita ilimaliza nafasi ya 10 ikiwa na pointi 34, ikicheza mechi 30, kushinda saba, sare 13, ikipoteza michezo 10, na ilisubiri mpaka mechi za mwisho ili kuhakikisha kama itasalia Ligi Kuu, kwani ilikuwa kwenye hatihati ya kushuka daraja au kwenda mechi za mchujo, 'play off'.



## ZISIKUPITE

### EDERSON OFA NENE

KLABU ya Manchester City imepokea dau la pauni milioni 25, kutoka kwa Saudi Pro League kwa ajili ya mlinda mlango wao, Brazil Ederson, 30. ***(HITC)***

### LINDELOF SOKONI

MANCHESTER United wanataka kumuuza mlinzi wa Sweden, Victor Lindelof, 29, msimu huu wa majira ya joto na pia watasikiliza ofa kwa ajili ya kiungo wa kati wa Denmark, Christian Eriksen, 32. ***(Manchester Evening News)***

### DOUE AGOMBEWA

CHELSEA ipo tayari kumenyana na Tottenham Hotspur, Bayern Munich na Paris St-Germain kumnunua kiungo wa kati Mfaransa Desire Doue, 19. ***(L'Equipe)***

### TAVARES MBIONI LAZIO

MLINZI wa Ureno, Nuno Tavares, 24, yuko mbioni kujiunga na Lazio kwa mkopo kutoka Arsenal. ***(Fabrizio Romano)***

### KUMFUATA MOURINHO

WINGA Mfaransa Allan Saint-Maximin, 27, anatarajiwa kuondoka Al-Ahli ili kuungana na Jose Mourinho huko Fenerbahce. ***(Yagız Sabuncuoglu)***

### TSYGANKOV ATAKIWA EPL

ARSENAL, Manchester United na Aston Villa wanamwania winga wa Girona na Ukraine, Viktor Tsygankov, 26. ***(AS)***

### TONEY AWANIWA UNITED

MANCHESTER United inavutiwa na mshambuliaji wa Brentford na England, Ivan Toney, 28, ambaye yuko tayari kuhamia Old Trafford. ***(Christian Falk via Mail)***

### VARANE ATIMKIA COMO

KLABU ya Como ya Italia iko tayari kumsajili mlinzi wa Ufaransa, Raphael Varane, 31, kama mchezaji huru baada ya kuondoka kwake Manchester United msimu huu. ***(Fabrizio Romano)***

### BERGWIJN AMULIKWA

WEST Ham imeonesha nia ya kutaka kumnunua winga wa Uholanzi, Steven Bergwijn, 26, lakini Marseille na Klabu za Saudi Arabia pia zinatumaini kumnasa kutoka Ajax. ***(De Telegraaf)***

### MORATA KUTUA MILAN

KLABU ya Atletico Madrid inatarajiwa kuipa AC Milan idhini ya kumsajili Alvaro Morata, 31, wiki ijayo baada ya kukamilisha majukumu yake ya kimataifa na Hispania kwenye Euro 2024. ***(Calciomercato)***

### GATTI AITAKA JUVE

EVERTON, West Ham na Newcastle United zinatazamiwa kumkosa Federico Gatti, 26, huku mlinzi huyo wa Italia akiwa tayari kuweka hatima yake kwa Juventus. ***(Tuttosport)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RUDIGER APEWA OFA YA BEKI GHALI ZAIDI

**Klabu anayocheza Ronaldo na ile ya Neymar zapigania saini yake huku...**

**MADRID,** Hispania

MLINZI wa Real Madrid, Antonio Rudiger, amepokea 'ofa nyingi' kutoka Saudi Arabia ambazo zitamfanya kuwa beki anayelipwa fedha nyingi zaidi katika soka duniani, kwa mujibu wa ESPN.

**Rudiger amejiimarisha kama mmoja wa mabeki wa kati wanaoongoza duniani katika miaka ya hivi karibuni, akifurahia misimu miwili ya mwisho katika Klabu ya Chelsea kabla ya kujiunga na Real Madrid kwa uhamisho wa bila malipo mwaka 2022.**

Baada ya msimu tulivu wa mechi ya kwanza Santiago Bernabeu, Rudiger alirejea katika kiwango chake bora zaidi wakati 'Los Blancos' hao waliposhinda Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2023/24, huku pia wakinyakua taji la LaLiga kutoka kwa wapinzani wao, Barcelona.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, anaendelea kuvutia umakini kutoka klabu za Ligi ya Saudia.

Inadaiwa kuwa timu mbili zinazoongoza ligi hiyo - Al Nassr, ambapo Cristiano Ronaldo anacheza soka la klabu yake, na Al Hilal ya Neymar - zitakuwa tayari kumlipa Rudiger mshahara utakaoweka rekodi ya dunia kwa mlinzi, na tayari ameshawekewa ofa mezani.


Hata hivyo, Rudiger ana mkataba na Madrid hadi 2026 na hana nia ya kuondoka. Vile vile, klabu inamwona kama mchezaji ambaye hatauzwa chini ya hali yoyote na mtu ambaye bado yuko katika mipango ya kocha, Carlo Ancelotti.

Madrid tayari wamemuona nahodha wa klabu hiyo Nacho Fernandez akiondoka kwenda kujiunga na Al-Qadsiah ya Saudia, huku David Alaba anaweza kuwa nje ya uwanja hadi 2025 wakati akiendelea kupata nafuu kutokana na jeraha la mguu.

Badala ya kuruhusu beki mwingine wa kati kuondoka, Madrid wanatafuta kuimarisha nafasi hiyo.

Walengwa wao wakuu ni Leny Yoro, lakini kwa wakati huu wanasitasita kufikia bei ya Lille ya euro milioni 50 - timu hiyo ya Ufaransa imekubali ofa kutoka kwa Manchester United, lakini mchezaji huyo bado hajaweka wazi mpango wa kuhamia Old Trafford.

# VARANE AONDOKA MAN UNITED



**MANCHESTER,** England

RAPHAEL Varane amekubali kujiunga na klabu ya Como ya Italia baada ya kumalizika kwa mkataba wake na Manchester United, ripoti imedai.

Mkataba wa Mfaransa huyo kule Old Trafford ulimalizika mwishoni mwa Juni na hakukubaliana na klabu hiyo juu ya maslahi mapya, hivyo kuhitimisha kukaa kwake kwa miaka mitatu England.

Varane alihusishwa na timu mbalimbali baada ya kuondoka United, lakini Fabrizio Romano anaripoti kuwa ametoa neno lake la kujiunga na Como.

Kuna maelezo kuhusu mkataba kufutwa, wakati Varane bado anatakiwa kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu, lakini mpango huo uko 'ukingoni' kukamilika.

Kocha msaidizi wa Como, Cesc Fabregas, anasemekana kuwa na mchango mkubwa katika kumshawishi Varane kujiunga na klabu hiyo.

Fabregas anatarajiwa kuendelea kufanya kazi chini ya usimamizi wa Osian Roberts, ambaye hivi karibuni alikataa nafasi ya kuinoa Timu ya Taifa ya Wales.

Roberts na Fabregas waliiongoza Como kupandishwa daraja hadi Serie A mwishoni mwa msimu wa 2023/24.

Varane hapo awali alisema angependa kuchezea moja ya klabu zake za zamani - Lens au Real Madrid - baada ya kuondoka United, lakini hakuna aliyejitokeza katika ofa hiyo.

Beki huyo wa kati aliondoka United akiwa amecheza mechi 95 katika kikosi cha 'Mashetani Wekundu' hao. Alichangia pia ushindi wao wa Kombe la Carabao na Kombe la FA katika misimu miwili chini ya Erik ten Hag.

# Navas atangaza kustaafu Hispania



**BERLIN,** Ujerumani

JESUS Navas amethibitisha kuwa fainali ya michuano ya Ulaya ya jana, Jumapili dhidi ya England mjini Berlin ilikuwa mechi yake ya mwisho kwa Hispania.

Navas mwenye umri wa miaka 38, ndiye pekee aliyebaki kwenye kikosi cha Hispania kilichoshinda Euro mara ya mwisho mwaka 2012.

Pia alikuwa sehemu ya timu iliyoshinda Kombe la Dunia mwaka 2010.

Ni jambo la kawaida kwa nahodha wa timu kuzungumza katika mkutano wa wanahabari kabla ya mchezo wa fainali, lakini fowadi wa Hispania, Alvaro Morata, alikabidhi jukumu hilo kwa Navas kutokana na kuwa mechi yake ya mwisho kwa nchi yake.

"Morata aliniambia ni wakati wa mimi kuzungumza kwa sababu utakuwa mchezo wangu wa mwisho," alisema Navas.

"Kuwa bado hapa baada ya miaka mingi inaonesha kuwa nimefanya mambo vizuri.

"Hata nikiwa na umri wa miaka 38, bado nina furaha kwa kila kitu, kusaidia timu ya taifa, nchi yangu ... lakini uamuzi umefanywa."

Navas aliichezea Hispania kwa mara ya kwanza mwaka 2009 na ameshinda mechi 56 katika miaka iliyofuata, zikiwamo tatu kwenye fainali za majira ya kiangazi nchini Ujerumani.

Alianza mchezo wa mwisho wa kundi dhidi ya Albania, aliingia akitokea benchi katika hatua ya 16 bora dhidi ya Georgia na kuanza katika ushindi wa nusu fainali dhidi ya Ufaransa akiwa beki wa kulia akichukua nafasi ya Dani Carvajal.

# Klopp arudishwa Liverpool

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amerejea tena Liverpool ikiwa ni miezi kadhaa tangu atangaze kuachana na timu hiyo na sasa amepewa cheo cha kuwa balozi wa heshima wa Taasisi ya Liverpool.

Klopp ambaye aliachana na Liverpool mwishoni mwa msimu uliopita ni miongoni mwa makocha waliopata mafanikio makubwa na timu hiyo akiiwezesha kushinda taji la Ligi ya Mabingwa na Ligi Kuu England na msimu wake wa mwisho aliisaidia kuchukua taji la Carabao.

Katika mchezo wa mwisho akiwa na Liverpool aliisaidia taasisi hiyo ambayo kazi yake ni kutoa misaada na kurudisha kwa jamii kukusanya jumla ya pauni milioni 40,000 ambazo zilitokana na mauzo ya vitu mbalimbali ambavyo aliweka saini yake.

Kocha huyu mwenye umri wa miaka 57, baada ya kuachana na Liverpool amekuwa akipokea ofa mbalimbali, lakini amesisitiza anataka kupumzika.

Baada ya kupewa ubalozi huo wa heshima Klopp alisema:"LFC Foundation inafanya kazi nzuri katika jamii kuanzia ndani ya Jiji la Liverpool na nje ya hapa, nina furaha sana ya kuendelea kufanya kazi nao, pia nashukuru kwa kuchaguliwa kuwa balozi wa kwanza wa heshima wa taasisi hii."

"Ninasubiri kuona nini tutafanya siku za usoni kwa sababu nina muda wa kutosha kwa sasa."

Matt Parish, ambaye ni Mtendaji Mkuu wa LFC Foundation naye alisema: "Tuna furaha kuendelea kushirikiana na Klopp ambaye atakuwa balozi wa kwanza wa heshima katika taasisi yetu, amekuwa akitusapoti sana katika nyanja mbalimbali na mapenzi yake na taasisi pamoja na Jiji la Liverpool ni makubwa sana."



## Gamondi awatumia ujumbe kina Chama

INATOKA UK. 24

sisi pamoja na kucheza soka safi lakini ni wapambanaji, napenda kuona wachezaji wangu wakipambana, yaani kama kufa ufie uwanjani ukiipigania nembo, na hicho nimeshaonyesha msimu uliopita," alisema.

Aliongeza, "ukiangalia baadhi ya mechi zetu za ligi tulikuwa tunapata ushindi dakika za mwisho kabisa, angalia tulivyocheza dhidi ya Al Ahly, CR Belouizdad na Mamelodi Sundowns, tulifanikiwa zaidi kwa sababu ya kupambana na hiyo ndiyo falsafa yangu ya mpira, yaani wote tunashambulia na wote tunakaba," alisema Gamondi.

Akizungumzia mechi ya Kombe la Toyota dhidi ya Kaizer Chiefs itakayochezwa, Julai 28, mwaka huu, nchini Afrika Kusini, alisema haitokuwa kipaumbele sana kwake, badala yake atatumia kuangalia ubora na ufiti wa wachezaji wake, wakiwamo wachezaji wapya, ili ajue pa kuanzia.

## Fadlu ajivunia kikosi Simba

INATOKA UK. 24

kwa mastraika wake ili wafunge mabao mengi kama alivyokuwa anafanya yeye enzi zake, ambapo ameshawahi kuwa mfungaji bora wa Ligi Kuu nchini Afrika Kusini mara mbili kwa nyakato tofauti wakati akicheza soka.

Wakati Simba ikiendelea kujifua nchini Misri jijini Dar es Salaam, Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa klabu hiyo, Crescentius Magori, amesema bado hawajamaliza usajili kama inavyofikiriwa.

Alisema bado wanaendelea na usajili ambao kwa mujibu wa Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), dirisha hilo linarajiwa kufungwa Agosti 15, mwaka huu.

"Bado, bado kabisa, usajili kwetu unaendelea, hatujamaliza," alisema Magori.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinaeleza kuwa, timu hiyo ipo kwenye mazungumzo na mchezaji Jonathan Alukwu kutoka Sporting Lagos ya Nigeria.

Mchezaji huyo anayecheza winga ya kushoto na wakati mwingine kiungo mshambuliaji, yupo karibuni kujiunga na kikosi hicho ili kuimarisha upande huo, baada ya upande wa kulia kumpata Jushua Mutale kutoka Power Dynamos ya Zambia.

# WAZIRI MKUU KUONGOZA DODOMA MARATHON, JEZI RASMI ZAZINDULIWA

**Na Mwandishi Wetu**

WARATIBU wa mbio za Dodoma Marathon wamezindua jezi rasmi zitakazotumiwa na washiriki wa mbio hizo zitakazofanyika Julai 28, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, mgeni rasmi akitarajiwa kuwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ambaye ataongoza washiriki zaidi ya 8,000 wa mbio hizo.

**Hafla ya kutambulisha jezi hizo imefanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki ambapo pia ilishuhudiwa mwandaaji huyo akitambulisha Kampuni ya Serengeti Breweries Limited (SBL), kama mshirika rasmi wa vinywaji na burudani kwenye tukio hilo.**

Lengo kuu la mbio hizo ni kukusanya fedha ili kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi na kutoa ufadhili wa elimu kwa wakunga ili kuboresha afya ya mama na mtoto.

Akizungumza kwenye hafla hiyo Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi ambao ndio waandaaji wa mbio hizo, alisema ubora wa jezi hizo pamoja na uwapo wa Waziri Mkuu kama mgeni rasmi wa mbio unatarajiwa kuongeza hamasa kwa washiriki hao kutoka makundi mbalimbali ya kijamii wakiwamo wakimbiaji kutoka taasisi na mashirika mbalimbali, wakimbiaji wa kimataifa, klabu mbalimbali za wakimbiaji nchini (Jogging clubs) na wakimbiaji mmoja mmoja, huku lengo likiwa ni kuunga mkono agenda kuu za mbio hiyo ya kuokoa maisha ya mama na mtoto.

"Pamoja na ubora na mvuto wa jezi zitakazotumika kwenye mbio hizi sambamba na uwapo wa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambaye kimsingi amekuwa nasi mara kadhaa kwenye mbio hizi, tunaamini mambo yatakuwa mazuri zaidi. Akizungumzia ubora wa jezi hizo zenye rangi tano tofauti, bluu, njano, nyeupe, nyekundu na nyeusi, Mkuu wa Idara ya Masoko wa NBC, David Raymond, alisema tofauti ya rangi hizo ambazo zimebeba maana tofauti inalenga kutoa chaguzi tofauti kwa kuzingatia tafsiri ya rangi na mtindo (design) ya jezi husika lengo likiwa ni kuhakikisha kila mshiriki anaridhika na kufurahia aina ya jezi atakayovaa kwenye mbio hizo.

"Ubora na ubunifu wa jezi hizi ulizingatiwa kwa kiasi kikubwa ambapo tumejitahidi kuziwekea alama mbalimbali zinazolenga kujenga maana, kuongeza mvuto na muhimu kuliko vyote tumeziwekea alama ya mng'ao maalum (reflectors) kwa ajili ya usalama wao wanapokuwa barabarani hususan nyakati za usiku wanapofanya mazoezi hata baada ya mbio," alibainisha.

Akizungumzia ushiriki wa mbio hizo, Raymond aliwaomba washiriki waendelee kujisajili na kuchangia kiasi cha Sh. 35,000 kwa usajili wa washiriki mmoja mmoja au 25,000 kwa usajili wa kikundi chenye idadi ya watu wanaozidi 25.

"Pia tunafarijika zaidi kuona kwamba wadau mbalimbali wanaendelea kujitokeza ili kutuunga mkono kwenye mbio hizi ambapo hii leo tunaitambulisha Serengeti Breweries kupitia kinywaji chao cha Captain Morgan kama mshirika mkuu wa vinywaji na burudani kabla na wakati wa tukio hilo," alisema Sabi .

Aidha, aliwashukuru wadau mbalimbali yakiwamo mashirika na kampuni zilizoshiriki kufanikisha mbio hizo.



Baadhi ya wageni waalikwa wakipata vinywaji mbalimbali kutoka kwa wahudumu wakati wa hafla ya utambulisho wa jezi zitakazotumika kwenye mbio za Dodoma Marathon 2024 jijini Dar es Salaam jana. Mbio hizo zitafanyika jijini Dodoma Julai 28. **MPIGAPICHA WETU**

# KMC yanasa kipa wa Biashara United

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya golikipa wao, Denis Richard, kuchukuliwa na JKT Tanzania, timu ya KMC nayo imelipa kisasi na kwenda kumchukua kipa wa Biashara United, Ismail Mpaki.

Ofisa Habari wa timu hiyo, Khalid Chukuchuku, amesema jana kuwa, usajili wa kipa huyo ni moja kati ya mikakati ya kujiimarisha vema na Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

"Tumemsajili kipa huyu kutoka Biashara United, ni kipa mzuri, benchi la ufundi limeridhishwa naye na tuna matgemeo makubwa kwake kwa sababu tumekiona kiwango chake akiwa na timu yake ya zamani," alisema Chukuchuku.

Kipa huyo ndiye aliyeidakia Biashara United katika mechi nyingi za Ligi ya Championship msimu uliopita, na hata michezo ya 'play off', ambapo nusura aipandishe Ligi Kuu, kama si kufungwa mabao 2-0 dhidi ya Tabora United katika mechi ya mkondo wa pili ya mchujo, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora, baada ya ushindi wa bao 1-0, Uwanja wa Karume, Musoma, Mara.

Mpaki, anakuwa ni mchezaji wa saba kusajiliwa na KMC, ambapo tayari imeshawatangaza, Ajoh Austin, straika kutoka Cameroon, Oscar Paul, kiungo mshambuliaji Mtanzania aliyekuwa akicheza soka la kulipwa nchini Kenya, katika Klabu ya Kakamega Home Boys, beki wa kati na Nickson Kassam Mosha, akitokea kikosi cha vijana cha Mtibwa Sugar.

Wengine ni kipa raia wa Burundi aliyekuwa akiidakia Klabu ya Vipers ya Uganda, Fabien Mutombora, Jean Nyezimana kutoka Vital'O ya Burundi na beki wa kati, Salum Athumani 'Stopper' kutoka KVZ ya Zanzibar.

Michezo

Jumatatu Julai 15, 2024

Nipashe



Klopp arudishwa Liverpool UKURASA 22





Kocha Miguel Gamondi akitoa maelekezo kwa wachezaji wake, Clautos Chama, Prince Dude, Keneddy Musonda wakiwa mazoezini Kigamboni. Kulia ni wachezaji wa Simba wapya mazoezini nchini Misri. **PICHA: WAPIGAPICHA WETU**

# Gamondi awatumia ujumbe kina Chama

**Na Adam Fungamwango**

## ● ● ● Asema hataangalia jina la mchezaji huku akitoa masharti ya kupata namba...

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amefichua kuwa katika falsafa yake ya mpira anapenda zaidi wachezaji wapambanaji wenye uwezo wa kushambulia na kukaba kwa wakati mmoja, huku akiendelea kusisitiza kuwa hatompanga mchezaji kwa sababu ya jina lake, bali kile anachokionyesha uwanjani.

**Katika dirisha hili kubwa, Yanga imewasajili wachezaji kadhaa akiwamo, Clatous Chama kutoka Simba, Prince Dube akitokea Azam FC, Aziz Andambwile (Singida Fountain Gate), golikipa Khomeiny Aboubakar na Duke Abuya (wote kutoka, Singida Black Stars), na Chadrack Boka kutoka FC Saint Eloi Lupopo ya DR Congo.**

Akizungumza wakati wa mazoezi ya timu hiyo, kocha huyo alisema yeye ni raia wa Argentina, lakini ana asili ya Italia, ambapo nchi zote hizo hupenda kucheza soka safi, lakini wana asilia ya upambanaji na kucheza kwa 'jihadi' kwa ajili ya kusaka ushindi.

"Msimu uliopita tulicheza vema, tulifunga mabao mengi na kushinda michezo mingi, msimu huu tumesajili wachezaji wengine wazuri na bora, kwangu mimi naona vizuri kwa sababu watapambana mazoezini ili kunionyesha ubora wao, ila nidhamu ndiyo ufunguo wa mafanikio, kwangu mimi nataka kuona kila mchezaji anapambana kupata namba.

"Mimi siangalii jina la mtu, hili narudia tena na tena, naangalia anafanya nini uwanjani, anaweza kuletwa mchezaji mwenye jina kubwa, lakini linatakiwa jina hilo lifanye kitu ndani uwanja, watu wanaweza kusema kocha ana machaguo mengi sana, lakini anachoangalia ni kikosi chake cha kwanza kinachompa matokeo bora," alisema Gamondi.

Kuhusu falsafa ya soka lake alisema yeye binafsi anapenda sana wachezaji wenye uwezo mkubwa wa kujitoa na kupambana kwa ajili ya timu.

"Mimi nimetoka Argentina, lakini nina asili ya Italia, hivyo

INAENDELEA UKURASA 23

# Fadlu ajivunia kikosi Simba SC

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Klabu ya Simba ikisema haijamaliza kufanya usajili wake kuelekea msimu ujao, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Fadluraghman Davids 'Fadlu', amesema anataka kutengeneza kikosi cha wachezaji wenye kiu, njaa ya ushindi na mafanikio, huku msingi wake ukiwa ni ushambuliaji zaidi.

Akizungumza wakati akiwa Ismailia nchini Misri ambako kikosi hicho kimeweka kambi kujiandaa na msimu ujao wa mashindano, kocha huyo raia wa Afrika Kusini, ambaye amepewa jukumu la kukinoa, akiwa mpya, na wachezaji wengi wapya, amesema pamoja na kuwafundisha mifumo ya uchezaji na staili mbalimbali, lakini anataka kuwajenga wachezaji wake wawe watu wa kupambana kusaka ushindi kwa nguvu na hali yoyote wanapokuwa uwanjani.

"Timu hii ina mashabiki wengi sana, kwa hiyo haiwezekani wachezaji wawe wanacheza tu kama kujifurahisha, nataka wawe wanacheza kwa malengo, wakipambana, wakitumia mafunzo tunayowapa wakichanganya na vipaji vyao kwa ajili ya kupambania nembo ya klabu na kuwajali mashabiki wao waliowafuata. Na hakuna kingine bali ni kucheza kwa kushambulia kwa kasi na kusaka ushindi, hili ni lazima likae kichwani mwa wachezaji wangu," alisema kocha huyo maarufu kwa jina la Fadlu.

Tayari kocha huyo alishabainisha kuwa anataka kutengeneza safu moja kali ya ushambuliaji ambayo itakuwa inafunga mabao mengi ili kushinda mchezo wa mpira wa miguu, kwani alisema usipofunga, basi ni lazima utatoka sare au kufungwa.

Alisema ili kufanya hivyo ni lazima atengeneze muunganiko, maelewano, mikimbio ya kusaka nafasi, mawasiliano ya mdomo na mwili

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >